
# Kuwatambua na kuwasaidia wanafunzi walio nje ya skuli

Module

3




## Muongozo wa mwezeshaji

Umetayarishwa kwa ajili ya:
Jumuiya ya MECP-Z na Jumuiya za Watu wenye Ulemavu
The Norwegian Association of Disabled
Umetayarishwa na:
Enabling Education Network

NAD – The Norwegian Association of Disabled
MADRASA EARLY CHILDHOOD PROGRAMME
EENET
Inclusive Learning Approach
SHIJUWAZA

[Maelezo ya picha: Mwanafunzi wa kiume aliyevaa sare za skuli, akiwa amebeba mkoba wa skuli mgongoni anapanda ngazi. Juu ya ngazi pameandikwa 'Skuli ya Sekondari'. Watoto watatu wamesimama chini ya ngazi. Watoto hao ni pamoja na mtoto wa kiume aliyevaa shuka aliyoifunga kiunoni akimuangalia mtoto mwengine wa kiume, mtoto mwengine wa kike aliyembeba mtoto mchanga mgongoni akionekana mwenye huzuni, na mtoto mwengine wa kiume aliyevaa miwani myeusi, akiwa ameshika fimbo akiangalia upande mwengine. Chini ya ngazi pameandikwa 'Skuli ya Msingi'.]

Kazi hii ina hadhi ya kibali cha Creative Commons Attribution Non-Commercial-Share Alike 4.0 International License. Si kwa ajili ya biashara. Kuangalia kivuli cha kibali hicho, tembelea tovuti ya
http://creativecommons.org/licenses/by-nc-sa/4.0/

# Yaliyomo


Utangulizi....................................................................................................5

Somo la 1: Utangulizi kuhusu wanafunzi walio nje ya skuli ................................7

Somo la 2: Kutatua tatizo la watoto walio nje ya skuli kwa kutumia sera zenye mkabala wa haki ..................................................................................15

Somo la 3: Kwa nini kuna watoto walio nje ya skuli Zanzibar? ..........................20

Somo la 4: Nini maana ya uhamaji katika taasisi za elimu na kwa nini ni muhimu? ................................................................................29

Somo la 5: Uhamaji jumuishi unaanzia nyumbani ..........................................34

Somo la 6: Jukumu la Jumuiya za Watu wenye Ulemavu katika kuwatambua wanafunzi walio nje ya skuli na kusaidia uhamaji jumuishi ..............................48

Kielelezo nam. 1.1: Ufafanuzi wa vipengele: Ni nani wanafunzi walio nje ya skuli na kwa nini wapo nje? ....................................................................60

Kielelezo nam. 1.2: Vikwazo vinavyohusina ....................................................68

Kielelezo nam 1.3a: Orodha ya vikwazo vinavyowazuia wanafunzi kujifunza...69

Kielelezo nam. 1.3b: Picha ya vikwazo vinavyowazuia wanafunzi kujifunza .....70

Kielelezo nam. 2.1: Picha za sera...................................................................86

Nyenzo: 2.2: Sheria na Sera za haki ya elimu Zanzibar .....................................87

Kielelezo nam. 3.1: Kadi za almasi 9 – Vikwazo vinavyowazuia wanafunzi kwenda skuli ..........................................................................92

Nyenzo 3.2: Visa mafunzo vinavyowahusu wanafunzi walio nje ya skuli..........93

Kielelezo nam. 3.3: Mikakati na suluhisho la kuwatafuta na kuwatambua wanafunzi walio nje ya skuli..........................................................96

Kielelezo nam. 4.1: Maelezo ya video ya 'Uhamaji jumuishi' iliyoandaliwa na EENET: Kwa nini uhamaji ni jambo linalotiliwa maanani katika elimu mjumuisho?.............................................................................97

Kielelezo nam. 4.2: Nini maana ya uhamaji katika taasisi za elimu?.................99

Kielelezo nam. 4.3: Walichosema wanafunzi kuhusu uhamaji .......................101

Kielelezo nam. 5.2a: uhamaji jumuishi huanzia nyumbani ............................102

Kielelezo nam. 5.2b: Seti ya picha tatu za mikakati .......................................104

Kielelezo nam. 5.3a: Mambo yanayoathiri uhamaji kabla ya kujiunga na skuli ........................................ 110
Kielelezo nam. 5.3b: Maelezo ya video ya 'Kabla ya kufika skuli' iliyoandaliwa na EENET........................................ 111
Kitini nam. 6.1: Kutumia sera kushawishi mabadiliko........................................ 114
Kielelezo nam. 6.2a: Simulizi ya Amina ........................................ 117
Kielelezo nam. 6.2b: Simulizi ya Yasmin ........................................ 118
Kielelezo nam. 6.2: Misingi ya kuzingatia ili kufanikisha uhamaji usio na usumbufu ........................................ 119
Kielelezo nam. 6.3a: Kadi za changamoto ........................................ 120
Kielelezo nam. 6.3b: Kadi za mikakati ........................................ 122

# Utangulizi

Moduli hii ina malengo mawili ya msingi.

Lengo la kwanza, ni kutoa maelezo ya kina kwa Jumuiya za Watu wenye Ulemavu (OPDs) na wadau wengine, Ofisi za Elimu Wilaya (DEO), jumuiya za kijamii, Jumuiya Zisizo za Kiserikali (NGOs) na vikundi vya wazazi, kuhusu wanafunzi walio nje ya skuli kwa kuzingatia mifano ya ndani ya nchi na duniani kwa jumla. Inaangalia vikwazo na mambo mengine yanayosababisha wanafunzi wawe nje ya skuli, na mlolongo wa sababu na athari zinazotokana na wao kuwa nje ya skuli. Moduli hii inawasaidia washiriki kutambua, kutafakari na kujadili vikwazo vinavyozuia upatikanaji wa elimu kwa wanafunzi na kufahamu kwa undani tatizo la watoto walio nje ya skuli katika muktadha mpana wa haki za binaadamu.

Lengo la pili la moduli hii ni kuhamasisha utumiaji wa njia zenye ufanisi kwa skuli kuhakikisha wanafunzi walio nje ya skuli, na wengine wote wanapata usaidizi wanaouhitaji ili kuwa na mchakato wenye ufanisi na thabiti wa kurejea skuli. Uhamaji katika taasisi za elimu unaelezea wanafunzi wanaoondoka, kuwasili au wanaojiunga kwa mara ya kwanza na elimu. Wanafunzi wengi hufika skuli katika muda ulioratibiwa, kwa mfano kutoka nyumbani na kujiunga na skuli ya maandalizi (ECE), kutoka skuli ya maandalizi kwenda skuli ya msingi, kutoka skuli ya msingi kwenda sekondari, au kutoka sekondari na kujiunga na chuo au kuajiriwa. Ijapokuwa, kuna idadi kubwa ya wanafunzi pia huingia au kutoka katika mazingira haya ya elimu nje ya muda ulioratibiwa. Wanafunzi hawa ni pamoja na:

- Wanafunzi walio nje ya skuli wenye umri wa kuandikishwa skuli lakini hawajawahi kwenda skuli au walikabiliana na changamoto zilizofanya iwe vigumu kwao kubaki skuli au wameacha masomo. Hii huenda ilisababishwa na sababu tofauti. Kwa mfano:
    - sababu za kiuchumi/kifedha
    - masafa kutoka skuli
    - ndoa za mapema
    - wana mahitaji ya ziada ambayo skuli haiwezi kuyakidhi
    - wazazi wao/walezi wana uelewa mdogo juu ya umuhimu wa elimu
- Wanafunzi ambao familia zao zinahamahama (kwa mfano, wanaohama nchi au kutoka kijijini kwenda mjini kutafuta kazi au kuungana na familia

au familia za wafugaji wanaohamahama wakitembea kutafuta malisho ya mifugo).

- Wanafunzi waliolazimika kuhama (kwa mfano, waliolazimika kuhama kutokana na ukame au njaa au mafuriko, na watu waliolazimishwa kuondoka au kukimbia vurugu na wakawa wahamiaji wa ndani ya nchi au wakimbizi).
- Wanafunzi waliofukuzwa skuli.

Ni muhimu kusisitiza kwamba hakuna njia moja ya kuwajumuisha wanafunzi walio nje ya skuli au kuufanya mchakato wa uhamaji katika taasisi za elimu uwe jumuishi kikamilifu. Hii ni kwa sababu mapito ya kila mwanafunzi ya kuwa nje ya skuli, kabla ya kujiunga skuli au baina ya skuli ni tofauti. Kwa hivyo, kila skuli na jamii inayoizunguka inapaswa kuwa tayari kukabiliana na mabadiliko yanayotokea na kwa hivyo kubuni njia tofauti za kutatua changamoto hizo kwa mujibu wa mazingira ya eneo.

Uratibu wa vipindi vya masomo katika moduli hii ufanyike kwa kuzingatia moduli nyengine zilizomo kwenye mfululizo huu zilizoandaliwa kwa ajili ya kujenga uwezo kwa Jumuiya za Watu wenye Ulemavu. Pia iunganishwe na mafunzo waliyopatiwa walimu kama ni sehemu ya programu ya Mafunzo ya Elimu Jumuishi kwa Walimu (IETT) na mikakati ambayo skuli za majaribio imeiweka kuwatambuwa watoto walio nje ya skuli na kusaidia kipindi cha mpito kuwa jumuishi.

## Muda wa Mafunzo

Wakufunzi wayarekebishe mafunzo haya ili kuendana na mazingira yao na muda uliopo kwa ajili ya kuendesha mafunzo hayo. Wakufunzi wanaweza kuamua kutotumia mazoezi yote, au kufupisha baadhi ya mazoezi kama muda hautoshi, au kurefusha mazoezi iwapo washiriki wanahitaji muda zaidi ili waifahamu mada fulani.

Iwapo mazoezi yote yatafanywa, bila ya marekebisho yoyote, kufupisha au kurefusha, moduli hii inahitaji takribani saa 18 za mafunzo, yatakayofanyika kwa siku 3 mpaka 4, kwa kuetegemea idadi ya saa walizoamua kwa kila siku ya mafunzo, idadi na urefu wa muda wa mapumziko, n.k.

# Somo la 1: Utangulizi kuhusu wanafunzi walio nje ya skuli

## Ujumbe mahususi

Kuna wanafunzi wengi ambao hawahudhurii skuli duniani kote. Wanajulikana kama wanafunzi walio nje ya skuli. Kuna sababu nyingi zinazowafanya wasiende skuli kama vile masafa kutoka skuli, umasikini au migogoro na majanga..

## Maelezo ya awali kwa mkufunzi

**Duniani kote:** "Kuna watoto milioni 264 na vijana ambao hawaendi skuli..."[1]
**Zanzibar:** "Takribani thuluthi moja ya watoto walio kwenye umri wa kujiunga na skuli (4-15) wapo nje ya skuli, wengi wao wakiwa na umri mdogo kabisa"[2]

Wanafunzi walio nje ya skuli ni pamoja na wanafunzi ambao hawajawahi kuandikishwa skuli pamoja na walioacha masomo kabla ya kumaliza. UNESCO imewagawa wanafunzi hawa katika makundi matatu:

- waliochelewa kuandikishwa
- wanaoacha mapema
- Wasiosoma kabisa

Kuna namna tofauti za kuvigawa vikwazo vinavyosababisha wanafunzi wawe nje ya skuli. Baadhi ya vigawanyo hivi vinapishana, au vinahusiana na vyengine. Kwa mfano, iwapo mwanafunzi yupo nje ya skuli kwa sababu familia yake inahama kutoka sehemu moja kwenda nyengine, mchakato wa kuhama utatambuliwa kama ni kikwazo, lakini sababu kuu za familia kuhama inaweza kuwa ni umasikini, au labda mgogoro katika eneo lao, au vyote.

Mkufunzi asome **Kielelezo nam 1.1** kabla ya kusomesha somo hili. **Kielelezo nam. 1.1** kinaeleza kwa kina kuhusu vikwazo mbalimbali ambavyo vinasababisha wanafunzi wawe nje ya skuli na inaweza kukusaidia katika kipindi chote cha somo.

---

[1] UNESCO (2017) *Accountability in Education. Meeting our Commitments. Global Education Monitoring Report, 2017/18*, p.i. http://unesdoc.unesco.org/images/0025/002593/259338e.pdf

[2] Taarifa kutoka (DHS) (2015/16) taarifa na utafiti wa bajeti ya kaya
(HBS) (2014/15)d, uk. 27 imetolewa katika ripoti ya uwezo wa kuwapokea watoto walio nje ya skuli Zanzibar iliotolewa na UNICEF pamoja na Shirika la Milele na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar

### Katika somo hili washiriki:

- ü Watatafakari kuhusu sababu mbalimbali zinazosababisha wanafunzi wawe nje ya skuli
- ü Watafikiria sababu zinazohusiana zinazosababisha wanafunzi wawe nje ya skuli
- ü Wataangalia vikwazo maalumu vinavyowazuia wanafunzi kwenda skuli

## Zoezi la 1.1: Vikwazo vinavyowazuia wanafunzi kwenda skuli

1 dakika 45

Zoezi hili litawasaidia washiriki kutafakari na kujadili vikwazo vinavyowazuia wanafunzi kwenda skuli. Litapima uwelewa wa mshiriki kuhusu vkwazo hivyo.

### Maelekezo

- Wakumbushe washiriki kwamba tuliangalia vikwazo vinavyokabili elimu mjumuisho katika mafunzo mengine. Vikwazo vya ujumuishwaji ni vikwazo vinavyoathiri **mahudhurio** ya mwanafunzi skuli, **ushiriki** wao katika mchakato wa kujifunza, na **maendeleo** yao.
- Waulize washiriki iwapo wanakumbuka baadhi ya vikwazo hivyo. (Wanatakiwa waweze kutaja kwa mfano vikwazo vya kimazingira; vikwazo vya nyenzo; vikwazo vya kimtazamo; vikwazo vya kisera na vikwazo vya kiutekelezaji).
- Waambie washiriki kwamba katika moduli hii tutaangalia **vikwazo vinavyosababisha wanafunzi wawe nje ya skuli** tu – ijapokuwa vikwazo vingi vinalingana na vikwazo vya ujumuishwaji.
- Waombe washiriki wakae katika vikundi. Kila kikundi kiwe na katibu kwa ajili ya kuandikakinachojadiliwa.

**Pawapointi** **Somo la 1: slaidi 1: Maelezo (Utangulizi) kuhusu zoezi**

- Waombe washiriki katika vikundi vyao wajadili na kuandika vikwazo vingi kadiri inavyowezekana vinavyosababisha wanafunzi wawe nje ya skuli.
- Kwa kila kikwazo, au sababu inayopelekea mwanafunzi awe nje ya skuli, wafikirie mfano maalumu. Ikiwa umasikini au ulemavu umetajwa kuwa

kikwazo, washiriki wafikirie mfano maalumu wa kila kikwazo (angalia jeduwali lililopo hapa chini – au toweni mfano mmoja kama kikundi).

| **Kikwazo kinachozuia mwanafunzi kwenda skuli** | **Mfano** |
|---|---|
| Umasikini | Kutoweza kumudu vifaa vya skuli, sare ya skuli au ada ya skuli |
| Mtazamo dhidi ya ulemavu | Wazazi wanaona aibu na wanamficha mtoto wao nyumbani |

- Baada ya dakika 15, omba kupatiwa mrejesho kutoka katika kila kikundi na uandike majibu yao kwenye flipchati. Kikwazo kimoja kinapotajwa, kikundi chengine kiombwe kutaja kikwazo tofauti (yaani, wasirejee kikwazo ambacho kimeshatajwa). Kila kikundi kitowe mifano yao mahususi ili kufafanuwa majibu yao.
- Onesha majibu yaliyoandikwa katika flipchati ili washiriki wayakumbuke wakati wa kufanya mazoezi mengine katika somo hili na masomo mengine.

**Tanbihi kwa mkufunzi (muwezeshaji)**

Rejea baadhi ya nukta wakati au baada ya majadiliano. Utafiti kuhusu elimu jumuishi Zanzibar *au* vipengele vya OPD na IETT vya programu ya TOFI vimebaini sababu tofauti zinazoelezea kwa nini wanafunzi hawaendi skuli. Sababu hizo ni pamoja na:

- ukame
- ndoa ya mapema
- mtazamo dhidi ya wanafunzi wenye mahitaji ya ziada, jinsia, ukabila;
- ugonjwa, ulemavu na ukosefu wa huduma za marekebisho
- uraibu wa dawa za kulevya
- Kuishi mbali na skuli
- kuonewa
- mazingira ya kusoma yasio salama au kushindwa kusafiri kwa usalama kwenda skuli
- afya dhaifu
- kutoka katika jamii inayobaguliwa ambayo hubaguliwa hata kwenye mfumo wa elimu na afya
- kuwa masikini
- ajira za utotoni; na
- Kuwa yatima.

Sisistiza kwamba wanafunzi walio nje ya skuli:

- hawajawahi kwenda skuli, au
- wameacha kabla ya kumaliza, au
- wakati mwengine wanakwenda skuli na wakati mwengine hawaendi.

## Zoezi la 1.2: Mchezo wa 'lakini kwa nini'

1 dakika 45

Zoezi hili litawasaidia washiriki kufikiria kuhusu sababu na madhara yanayopelekea mwanafunzi kutokuwepo skuli.

### Maelekezo

**Pawapointi** **Somo la 1: slaidi ya 2: Mchezo wa 'lakini kwa nini'**

- Waambie washiriki yafuatayo:

  Hii ni simulizi inayomuhusu mtoto wa kike mwenye umri wa miaka nane anayeitwa Maryam. Maryam anaishi katika Kijiji kilichoko mbali. Kijiji chao hakina skuli, na hajawahi kwenda skuli. Kwa nini Maryam yupo nje ya skuli?
- Weka 'lakini kwa nini' kama ni kichwa cha habari katika flipchati.
- Halafu ongoza mjadala ambao unawahamasisha washiriki kufikiria mambo yanayosababisha Maryam awepo nje ya skuli. Kwa mfano:

Jibu la mshiriki: "Kwa sababu hakuna skuli kijijini kwao". Andika jibu hilo kwenye flipchati chini ya neno 'kwa nini'

Jibu la mkufunzi: "**Lakini kwa nini** hakuna skuli kijijini kwao**". Andika 'lakini kwa nini'** nyengine chini ya jibu **'Kwa sababu hakuna skuli kijijini kwao'.**

Jibu la mshiriki: "Inawezekana labda kwa sababu Kijiji chao ni masikini". Andika jibu hilo chini ya 'Lakini kwa nini' ya pili.

Jibu la mkufunzi: "**Lakini kwa nini** kijiji chao ni masikini?" na andika 'Lakini kwa nini' nyengine chini ya jibu 'Labda kwa sababu Kijiji chao ni masikini'.

Jibu la mshiriki: "Kwa sababu kijiji chao kipo mbali vilimani". Andika majibu haya kwenye flipchati chini ya neno 'Lakini kwa nini' la mwisho.

Jibu la mkufunzi: "**Lakini kwa nini** kijiji hicho kilichopo mbali vilimani ni masikini?" Andika 'Lakini kwa nini' nyengine kwenye flipchati.

- Endelea na utaratibu huu wa kuuliza maswali, ili kuwawezesha washiriki kuzama katika uchambuzi wa kina wa sababu kuu za kijamii, kimazingira na kisiasa zilizomfanya Maryan awe nje ya skuli.
- Flipchati itawasaidia washiriki kuufahamu vizuri mchezo. Wahamasishe washiriki kufikiria sababu nyingi kadiri inavyowezekama zilizosababisha Maryan awe nje ya skuli. Hii itawasaidia washiriki kufikiria kwa kina zaidi mbali na sababu nyepesi zinazosababisha wanafunzi wawe nje ya skuli, sababu nzito zaidi na hata sababu zenye uhusiano.

**Pawapointi** **Somo la 1: slaidi ya 3 na 4: Vikwazo vinavyohusiana vinavyokwamisha wakufunzi kwenda skuli**

- Waeleze washiriki:

  "Mchezo wa 'Lakini kwa nini' ni mchezo unaotuwezesha kuchambua matatizo ambayo utatuzi wake ni mgumu ambayo yanasababishwa na mambo mengi na tofauti. Kutambua chimbuko la matatizo hayo na kufahamu uhusiano uliopo baina yao kutatusaidia kujiandaa kuyatafutia suluhisho. Hii ni aina mojawapo ya kufikiri kwa makini. Mchezo huu una umuhimu kwetu tunapojiandaa kutafakari kwa kina vikwazo mbalimbali vinavyowazuia wanafunzi kwenda skuli".

- Onesha slaidi 4 (mfano wa mchoro wa vikwazo vyenye uhusiano) na/au wape **Kielelezo nam. 1.2** na waeleze kwamba badala ya kufikiria kuna sababu moja nyepesi  ya kumfanya mwanafunzi awe nje ya skuli, kiuhalisia kuna sababu nyingi zinazoweza kuchangia uwepo wa tatizo hilo.

  "Kwa mfano, uhaba wa walimu waliopatiwa mafunzo sahihi unaweza kupelekea skuli kuwa na walimu wachache, wenye taaluma duni na madarasa yenye idadi kubwa ya wanafunzi. Hii itapelekea wanafunzi kupata elimu duni. Hii inaweza kuwasababishia kuacha skuli kwa sababu hawasomi, na/au wazazi wao au walezi wanahisi haina maana kuwapeleka skuli. Skuli pia inaweza kuwa mbali na anakoishi mwanafunzi jambo ambalo litaathiri mahudhurio ya mwanafunzi."

- Chora wakati unatowa maelezo haya ili kuwawezesha kuona taswira halisi kwa mchezo huu ijapokuwa mara hii unaunganisha tu sababu na mishale kwenye flipchati.
- Omba mrejesho kuhusu mchezo huo kutoka kwa washiriki.
- Waambie washiriki kwamba wana dakika tano (5) kila mmoja za kufikiri na kubuni hadithi zao wenyewe za 'Lakini kwa nini', kwa kutumia simulizi ya Maryan kama mfano. Wanaweza kuandika wakijisikia kufanya hivyo. Flipchati mbili ulizoziandika zitawasaidia kuona kile wanachotakiwa kukifanya na wao.
- Hatua inayofuata, wagawe washiriki wakae **wawiliwaili** na waombe kwa zamu wacheze mchezo huo kwa kutumia simulizi ya kila mmoja wao ya 'Lakini kwa nini'. Zoezi hili lifanyike kwa dakika kumi (10).
- Simamia kipindi kifupi cha dakika 5 cha mjadala wa kutoa mrejesho.

## Zoezi la 1.3: Kuelezea maana ya wanafunzi walio nje ya skuli – vikwazo na sababu

1 dakika 30

### Maelekezo

- Eleza kwamba, kuna aina mbalimbali za vikwazo vinavyowazuia wanafunzi kwenda skuli ambapo ndani ya vikwazo hivi tunaweza kubaini vikwazo maalumu. Changamoto kuu zimegawanywa katika aina kuu tatu:

| Mzingira na vifaa/nyenzo | Mitazamo na imani | Sera na utendaji |
|---|---|---|
| | | |

- Chora jeduwali la aina tatu kuu mapema katika karatasi tatu tofauti za flipchati, huku ukiacha nafasi ya kutosha kwa ajili ya kuandika mifano chini ya kila aina ya vikwazo.
- Wapange washiriki katika vikundi vya watu 4-5. Gawa kwa kila kikundi nakla ya **Kielelezo nam. 1.3a: Muhutasari wa vikwazo vinavyomzuia**

**mwanafunzi asiende skuli,** ukionesha baadhi ya aina za vikwazo vinvysababisha wanafunzi wawe nje ya skuli, na pia mifano ya vikwazo maalumu.

- Waoneshe washiriki katika kila kikundi picha iliopo katika **Kielelezo nam. 1.3b.** Waambie washiriki kuwa kila mojawapo kati ya hizi inawakilisha vikwazo vinavyozuia washiriki kwenda skuli.

**Pawapointi**

**Somo la 1: slaidi ya 5: Ugawaji wa vikwazo**

- Watake washiriki katika vikundi vyao kuangalia vitini (maneno na picha) na kujikumbusha vikwazo walivyoorodhesha wakati wa **Zoezi 1.1** (waoneshe orodha ya vikwazo walivyonakili kutoka kwenye flipchati wakati wa zoezi), na wajadili maswali yafuatayo:
  - **Kikwazo kipi kinalingana na aina gani?**
  - **Je! Unaweza kutoa mfano (halisi)?**
- Baada ya dakika 15, viombe vikundi kuandika Mawazo yao na wabandike picha zao katika flipchati ukutani chini ya aina tofauti.
- Simamia majadiliano, ukihakikisha kwamba kila aina inazungumziwa wakati wa mjadala. Karibisha mifano halisi, mifano hii inaweza kutolewana washiriki au uzoefu wa mkufunzi na mawazo yaliyopo katika **Kilelezo nam. 1.1.**
- Waoneshe kuwa vikwazo vinaweza na **huingiliana na aina tofauti, ikionesha ni jinsi gani vina tabia ya kuhusiana.**



Wakufunzi wakuu wakipitia aina za vikwazo

[Maelezo ya picha: Karatasi zimebandikwa ubaoni. Baadhi zimepewa majina ya aina za vikwazo (kwa mfano, wingi wa wanafunzi, ukosefu wa vifaa). Wanaume wawili wanaendelea na kazi ya kubandika orodha ya vikwazo katika ukuta.]

- Mkufunzi anaweza kuwasilisha slaidi ya PawaPointi (6-8) kwa kuzingatia maelezo yaliyotolewa katika **Kielelezo nam. 1.1,** kwa kutegemea kiasi gani cha maudhui kitakachojadiliwa wakati wa mjadala.

**Pawapointi** **Somo la 1: slaidi ya 6-8: Aina za vikwazo vinaavyowazuia wanafunzi kwenda skuli pamoja na michoro**

- Sisitiza kwamba zoezi hili linaangalia tatizo la wanafunzi walio nje ya skuli dunia nzima, ili kuwasaidia washiriki kujifunza aina tofauti za sababu zinazowazuia wanafunzi kwenda skuli duniani kote. Baadae tutaangalia kwa ukaribu jinsi tatizo hili linavyohusiana na hali ya Zanzibar katika mafunzo yetu. Kufahamu muktadha wa dunia nzima kunaweza kutusaidia sana tutakapokuwa tunajaribu kufahamu muktadha wetu wenyewe vizuri.

# Somo la 2: Kutatua tatizo la watoto walio nje ya skuli kwa kutumia sera zenye mkabala wa haki

**Ujumbe mahususi**

Kuna vikwazo vingi vinavyowazuia wanafunzi kwenda skuli. Lakini kwa upande wa Zanzibar, kama ilivyo katika nchi nyingi, elimu ni haki ya watoto wote. Ni muhimu kutambua sera zilizopo Zanzibar ambazo zinalinda haki ya watoto ya kupata elimu. Tunaweza kutumia sera hizi kuendesha harakati za utetezi wa kudai haki za watoto walio nje ya skuli. Lakini ili tuweze kuzitumia ipasavyo tunapaswa KUANGALIA zinasema nini na KUFIKIRIA jinsi ya kuzitumia vizuri.

## Taarifa za msingi kwa mkufunzi

- Somo lililopita liliwasaidia washiriki kufahamu na kutafakari kuhusu vikwazo vinavyowafanya wanafunzi wawe nje ya skuli. Vikwazo hivi vinatakiwa viondolewe.
- Hatua muhimu ya awali ya kufanya hivyo ni kufahamu ufikiaji wa elimu kama ni chombo cha haki na haki ya binadamu kilichopo Zanzibar ambacho kinalinda haki hii.
- Lakini kufahamu tatizo la kuwa nje ya skuli kama ni ukiukwaji wa haki ya elimu kwa watoto hawa haitoshi. Tunapaswa kufikiria ni jinsi gani tunaweza kutumia haki za binadamu kufanya utetezi kwa ajili ya haki za watoto walio nje ya skuli.
- Ili kuweza kutumia nyenzo hii ya haki za binadamu ipasavyo tunapaswa kuangalia kwa kina sera muhimu zinasemaje.

## Katika somo hili washiriki:

- ü Kutafakari maana ya sera na aina zake.
- ü Kuziangalia sera tatu za Zanzibar ambazo ni muhimu katika kulinda haki ya watoto ya elimu.

## Zoezi la 2.1: Nini maana ya sera?

1 dakika 30

### Maelekezo

- Waombe washiriki wajigawe katika wawiliwawili.

**Pawapointi** **Somo 2: Nini maana ya sera?**

- Onesha **Slaidi 1 ya PawaPointi ya Somo la 2.** Waombe washiriki wajadili katika jozi zao swali lililooneshwa katika slaidi, **Nini maana ya sera?** Wape dakika 10 za kujadiliana.
- **Baadae waombe, wajadili kwa nini tuna sera. Wape dakika 5.**
- Sasa onesha **slaidi ya 2 - 3 ya PawaPointi ya Somo la 2.** Wape nakala ya **Kielelezo nam. 2.1: Picha za sera** kwa kila jozi na waombe waziangalie picha zote 3 na wajadili maswali:
    - o **Picha ipi katika picha ulizopewa ni ya sera?**
    - o **Kwa nini unasema hivyo?**
    - o **Kuna yoyote miongoni mwa picha hizo ambayo si sera?**
    - o **Kwa nini unasema hivyo?**
- Wape dakika 10 kujadili picha hizo 3. Wakumbushe washiriki kusoma maelezo ya picha iwapo kuna mshiriki yeyote asiyeona.
- Wakati wa mjadala, pokea baadhi ya michango ya jumla na mrejesho.
- Waoneshe **slaidi ya 4-5 ya PawaPointi** na wasomee nukta kuu:

**Kuna aina tofauti za sera**

ü Sera inaweza kuwa ni seti ya *misingi ya kazi* iliowekwa kwa ajili ya kukiongoza kikundi cha watu au taasisi (kwa mfano, sera ya skuli inayotoa muongozo kuhusu mwalimu asiyefika skuli au kanuni zinazoongoza kikundi cha vijana)

ü Sera inaweza kuwa ni seti ya *mikakati* ambayo serikali inapanga kuitekeleza ili kuleta mabadiliko ya namna fulani (kwa mfano, sera ya elimu mjumuisho)

ü Sera inaweza kuwa ni *sheria* ambayo inaongoza mfumo wa sheria wananchi (kwa mfano, sheria ambayo inawalinda watu kutokana na

ubaguzi)

- ü Jambo la kuzingatia ni kwamba, sera *inaashiria nia* na muongozo ambao serikali au taasisi inawataka watu wake kuufuata na kuutekeleza. Sera inayowapa watoto haki ya elimu inaashiria kwamba serikali inawathamini watoto wote na ingependa kuona wote wanapata elimu. Sera inayopinga ukatili katika skuli inaashiria kwamba skuli haitovumilia kitendo cha kuwadhuru wanafunzi na inataka wanafunzi wote wajisikie salama na wenye kuthaminiwa na kwamba wale wenye nia ya kukiuka sera hii watachukuliwa hatua.
- ü Sera zinaweza kufanya kazi katika ngazi tofauti (kwa mfano, zinaweza kuongoza utekelezaji katika ngazi ya skuli au zinaweza kufanya kazi katika ngazi ya kimataifa kuziongoza nchi mbalimbali, kama vile Mkataba wa Umoja wa Mataifa wa Haki za Watu wenye Ulemavu)
- ü Sera zinaweza kuwa na malengo ya muda mfupi, muda wa kati au muda mrefu
- ü Sera tunazozisoma mara nyingi zina historia fulani – nani alihusika katika kuunda sera hiyo, kuna mambo ambayo watu walikuwa hawakubaliani na vipi walikubaliana kuhusu kile kinachozungumziwa na sera
- ü Kwa hivyo, tunapoinangalia sera tunapaswa KUIANGALIA na KUITAFAKARI kwa makini.

## Zoezi la 2.2: Kuzichambua sera zinazohusu haki ya elimu kwa watoto wote

1 dakika 60

### Maelekezo

- Waombe washiriki wajigawe katika makundi matatu. Wape washiriki wa kila kikundi moja ya sera iliopo katika **Kielelezo nam. 2.2: Sera zinazohuku haki ya elimu Zanzibar** (kila kikundi kiwe na sera tofauti).
- Onesha **slaidi ya 6 ya PawaPointi ya Somo la 2** na soma maelezo yaliyopo kwenye slaidi:

**Pawapointi** **Session 2: slide 6: instructions for activity 2.2**

Soma kwa umakini sehemu ya sera uliyopewa. Iwapo kuna watu katika kikundi chenu ambao hawaimudu vyema lugha ya Kiingereza na/au kiwango chao cha elimu ni kidogo, hakikisha kwamba kuna mtu kwenye kikundi ambae anaweza kuwafasiria/kuwaelezea kila kilicho ndani ya sera. Baadae mjadili maswali yafuatayo katika kikundi chenu.

Mtu mmoja awe mwandishi wa kikundi na achukuwe maelezo ya mtachokijadili.

- ü Sera inasemaje kuhusu haki ya elimu?
- ü Fikiria jamii yako na watoto ambao wapo nje ya skuli.
  - **Kuna vikwazo gani vilivyopo ambavyo vinaweza kufanya iwe vigumu kutekeleza haki ya elimu kwa watoto walio nje ya skuli?**
  - **Kuna rasilimali zozote ambazo zingeweza kusaidia upatikanaji wa haki ya elimu kwa watoto walio nje ya skuli?**

- Wape washiriki katika vikundi vyao takribani dakika 30 za kujadili maswali.
- Viombe vikundi kuripoti walichokijadili mbele ya washiriki wote (toa dakika 5 kwa kila kikundi).
- Uliza iwapo kuna mshiriki yeyote mwenye maswali au iwapo kuna mshiriki yeyote ambae angependa kutowa mchango wowote.
  - o Kulikuwa na ugumu wowote katika kutafakri kuhusu sera?
  - o Kuna sera nyengine ambazo washiriki wanaweza kuzikumbuka ambazo ni muhimu katika kulinda haki ya elimu ya watoto walio nje ya skuli? (Washiriki wanaweza kuzitaja zifuatazo: Mkataba wa Haki za Mtoto, Sera ya Elimu ya Zanzibar (2006) au mabadiliko yanayofanywa katika sera hiyo hivi sasa, Mkakati wa elimu (2020), Sera ya haki za watoto (2017).

### Tanbihi kwa mkufunzi

Zoezi hili ni kwa ajili ya k**ujifunza kuchunguza na kuchambua sera kwa undani** na kufikiria kuna changamoto gani katika kuzitekeleza sera hizo. Zoezi hili halihusu maudhui ya kila sera na pia hakuna majibu 'sahihi' au 'yasiyosahihi' kuhusu kitu gani kimezungumzwa na sera au hakijazungumzwa. Jaribu kuchagua na kufupisha nukta kutoka kwenye mjadala ambazo zinahusu uchambuzi wa sera na kufikiria kuhusu changamoto za utekelezaji.

Baadhi ya mambo yanayoweza kujitokeza ni:

- Lugha inayotumika katika uundaji wa sera mara nyingi ni vigumu kufahamika kwa urahisi na hii inafanya kuwa vigumu kuitumia sera vizuri. Ni muhimu tujadili kwa pamoja kilichozungumzwa katika sera pamoja na maana yake.
- Ijapokuwa sera inaweza kuwa ni nzuri sana na inazungumzia mambo mazuri sana, kuna changamoto nyingi za utekelezaji mzuri wa sera hizo.
- Wakati mwengine sera hazifahamiki vizuri kwa wale wanaohitajika kutekeleza sera hizo.

- Waambie washiriki kwamba tutajadili baadae jinsi gani tunaweza kutumia sera hizi kufanya utetezi wa haki za watoto walio nje ya skuli.

# Somo la 3: Kwa nini kuna watoto walio nje ya skuli Zanzibar?

## Taarifa za msingi kwa mkufunzi

Baada ya kuyaangalia makundi mbalimbali ya wanafunzi walio nje ya skuli, somo hili litawasaidia washiriki kutafakari wakiwalenga zaidi wanafunzi walio nje ya skuli kwa Zanzibar pekee. Kuna sababu nyingi zinazowafanya wanafunzi Zanzibar wasiende skuli, kuwa na mahudhurio duni au kuacha baada ya kuhudhuria kwa muda. Baadhi ya sababu hizo ni pamoja na mitazamo hasi, mazingira yasiofikika au ukosefu wa sera wezeshi. Pia kuna wanafunzi wengi walioacha skuli na hawakurejea tena zilipofunguliwa baada ya kufungwa kwa kipindi kirefu kutokana na janga la UVIKO-19. Kwa mfano, watoto wa kike ambao walilazimishwa kuolewa/ndoa ya mapema, walipata ujauzito na hivi sasa ni mama au watoto wa kiume ambao walitafuta kazi ili kuzisaidia familia zao.

## Katika somo hili washiriki:

- Watajadili sababu kuu zinazowafanya wanafunzi wawe nje ya skuli Zanzibar
- Wataeleza visa mafunzo vya kweli vinavyowahusu wanafunzi walio nje ya skuli kutoka katika mazingira yao
- Kuanza kutafakari kuhusu changamoto za kuwagundua na kuwatambua watoto walio nje ya skuli na mikakti tunayoweza kuitumia kutatua changamoto hizi

## Zoezi la 3.1: Kwa nini wanafunzi wapo nje ya skuli Zanzibar?

1 dakika 45

Zoezi hili linawasaidia washiriki kutafakari kuhusu aina za vikwazo vya kwenda skuli vinavyowakabili wanafunzi Zanzibar na jinsi gani vinavyojulikana. Kabla ya zoezi kuanza mkufunzi akate kadi za 'almasi 9' kutoka kwenye **Kielelezo nam. 3.1** (zikiwemo kadi zilizokuwa hazijaandikwa). Kila kikundi kinahitaji seti moja ya kadi, na zitiwe kwenye bahasha.

## Maelekezo


Waombe washiriki wafanye kazi katika vikundi vidogo. Vikundi hivi vinaweza kuwa ni vikundi vya wilaya katika ngazi ya taifa. Wape washiriki katika kila kikundi seti ya kadi za 'almasi 9', zikate kutoka kwenye **Kielelezo nam. 3.1.**

**Pawapointi** **Somo 3: slaidi 1-2: Maelekezo kwa ajili ya zoezi la 3.1**

- Waeleze washiriki katika kila kikundi kwamba wanapaswa kuchagua **kadi 9 katika kadi zilizopo** zilizokuwepo na kuzipanga mezani katika umbo la almasi zikionesha mpangilio kutoka mashuhuri zaidi kuelekea isiyo mashuhuri na vikwazo vyenye changamoto vinavyozuia wanafunzi kuwa skuli Zanzibar. Vikwazo vikubwa zaidi viwekwe juu na vikwazo vidogo vikae chini.
- Chora mchoro wa almasi 9 (chini) kwenye flipchati/ubao kuwaonesha washiriki jinsi ya kuzipanga kadi.

**Mchoro wa almasi 9**

vikubwa/vyenye changamoto zaidi



Vikwazo vidogo

- Waambie washiriki kuwa kuna **zaidi ya kadi tisa,** kwa hivyo washiriki wataamua kadi zipi wazitumie.
- Waambie washiriki kwamba pia kuna **kadi zisizo na maandishi.** Hakikisha kikundi kina kadi hizi pia. Wanakikundi wakitaka wanaweza kuandika vikwazo tofauti kwenye kadi zisizo na maandishi na kuzitumia katika mpangilio wao wa almasi 9.
- Waambie washiriki wanapaswa kukubaliana kuhusu mpangilio wa kadi katika kikundi. Zoezi hili lifanyike kwa dakika 15-20.



Washiriki wa Zanzibar wakifanya kazi ya kupanga mchoro wa almasi 9

[Maelezo ya picha: Vipande kadhaa vya karatasi vipo juu ya meza. Vinaelezea vitu kama vile lugha na mtazamo wa watu juu ya ulemavu. Ipo mikono minne juu ya meza. Mkono mmoja ndio unaotembea na kuvipanga vipande vya karatasi.]

- Baada ya vikundi kumaliza kupanga kadi zao, waelekeze washiriki kuzungukia meza nyengine na kila kikundi kielezee kwa vipi na kwa nini walizipanga kadi zao katika mpangilio huo. Zoezi hili lichukuwe dakika 20-25.


16 Wakufunzi wakuu wakijadili mpangilio wa kila kikundi wa almasi 9

[Maelezo ya picha: Wanawake watatu na mwanaume mmoja wamesimama karibu na meza. Juu ya meza kuna vipande vidogo vya karatasi vyenye maandiko, ambavyo washiriki wanaonekana kujadili.]

- Shirikiana na washiriki wakitembea kutoka kikundi kimoja kwenda chengine, kuwahamasisha washiriki kuuliza maswali na kusaidia mijadala ifanyike kwa utulivu.
- Fikiria namna ya kurekodi almasi 9 za vikundi na majadiliano (kwa mfano, piga picha mpangilio wa almasi 9 na andika muelekeo wa mijadala ya vikundi kwenye flipchati/ubaoni).

## Zoezi la 3.2a: Kuangalia visa mafunzo – sehemu ya 1

1 dakika 45

- Fanya kichangamshaji cha haraka ili kuwapanga washiriki katika vikundi vipya.
- Wape washiriki wa kila kikundi kisa mafunzo cha mwanafunzi aliye nje ya skuli katika mazingira ya Zanzibar.

**Tanbihi kwa mkufunzi**

Unaweza kutoa kisa mkasa kimoja au viwili kwa kila kikundi ili kuhakikisha kwamba kuna visa mkasa vingi vinavyozungumziwa kadiri iwezekanavyo. Unaweza kuamua mwenyewe utumie visa mkasa gani.

**Pawapointi** **Somo 3: slaidi 3: Maelekezo kwa ajili ya zoezi 3.2a**

- Waambie washiriki, katika vikundi vyao, kujadili:
  - ü Kwa nini mwanafunzi yupo je ya skuli (kwa mfano, ikiwa mwanafunzi amaeacha skuli, huhudhuria mara chache au hajawahi kwenda skuli).
  - ü Kuna vikwazo vipo vinavyomzuia mwanafunzi kwenda skuli, ikiwemo maelezo kuhusu familia ya mtoto, mahali, kabila, uzoefu katika elimu, n.k.
  - ü Kwa namna gani vikwazo hivi vinaweza kuondoshwa? Njia zipi zinaweza kutumika kutatua tatizo hili?
- Waambie washiriki katika vikundi vyao kujadili kila kisa mkasa kwa dakika 15 na kunakili majibu yao kwenye karatasi ya flipchati. Wakimaliza kujadili kisa mkasa kimoja, wanaweza kuanza kujadili chengine.
- Katika kila mjadala, kila kikundi kitowe mrejesho wake na vikundi vyengine vinaweza kuchangia.
- Rudia hatua hiyo mpaka vikundi vyote vitakapomaliza kuwasilisha visa vyao.

## Zoezi la 3.2b: Kuangalia visa mkasa – sehemu 2

1 dakika 30

- Waombe washiriki kutoa mifano yoyote ya wanafunzi walio nje ya skuli Zanzibar waliowahi kuishuhudia au wanayoijua katika vikundi vyao. Washriki wanaotoka sehemu moja wanaweza kushirikiana katika vikundi kwa ajili ya zoezi hili. Mjadala ufanyike kwa takribani dakika 10.
- Hatua inayofuata waombe washiriki kukaa katika vikundi na kuchora na/au kuandika kisa mkasa kifupi **kinachomuelezea mwanafunzi aliye nje ya skuli *Zanzibar.*** Watakuwa na dakika 15-20 ya kufanya zoezi hilo. Ni vyema kisa mkasa kiwe cha kweli kinachomuhusu mwanafunzi aliye nje ya skuli ambae washiriki wanamjuwa.

**Pawapointi** **Somo la 3: slaidi ya 4: Maelekezo kwa ajili ya zoezi la 3.2b**

- Waambie washiriki kwamba kila kisa mafunzo kiandikwe kwenye karatasi ya flipchati ili kioneshwe, na kieleze:
  - **Kwa nini mwanafunzi yupo nje ya skuli, na iwapo mwanafunzi aliacha au hajawahi kwenda skuli**
  - **Kuna vikwazo gani vinavyomzuia mwanafunzi kwenda skuli, (zikiwemo taarifa sahihi kuhusu familia ya mwanafunzi, mahali, kabila, uzoefu wake kuhusu elimu, n.k.)**

  Vyenginevyo, washiriki wanaweza kujadiliana kwa kina na kujiandaa kusimulia kisa hicho.
- Wakati vikundi vinajadiliana kuhusu visa vyao, mkufunzi azunguke katika ukumbi akiangalia na kuandika maelezo kuhusu kisa fulani ambacho kitapendeza zaidi kukijadili wakati wa majadiliano.
- Baadae visa vipya vibandikwe ukutani ili washiriki wote waweze kuvisoma.

## Zoezi la 3.3: Mbinu na namna ya kuwapata na kuwabaini wanafunzi walio nje ya skuli

1 dakika 60

Zoezi hili limekusudiwa kuwafanya washiriki kufikiria changamoto ya kuwapata na kuwatambua wanafunzi walio nje ya skuli Zanzibar na kufikiria mikakati inayoweza kutumika kutatua changamoto hizi.

### Maelekezo

- Wakumbushe washiriki kwamba tumeangalia kwa nini watoto **Zanzibar** wapo nje ya skuli na vikwazo wanavyoweza kukabiliana navyo wakitaka kurudi skuli na kudumu huko. Tuliangalia sera zinazolinda haki yao ya elimu.
- Waambie washiriki kuwa hata kama tunajuwa kwa nini watoto wapo nje ya skuli na aina ya vikwazo vinavyowakabili, hatujui watoto hawa wanapatikana wapi ndani ya jami zetu na vikwazo maalumu wanavyokabiliana navyo. Kwa hivyo, ni muhimu kutafuta namna ya kuwapata na kuwatambua wanafunzi walio nje ya skuli katika jamii. Baada yah apo tunaweza kuandaa mikakati ya kuwarudisha skuli. Tunaweza kutumia mzunguko wa ANGALIA, TAFAKARI, TENDA kufanya hili.
- Waambie washiriki kuwa hivi sasa tutaangalia njia za kuwapata na kuwatambua katika jamii zetu ili tuandae mikakati ya kuwarudisha skuli.
- Waombe washiriki wakae katika vikundi vilevile walivyokuwemo katika zoezi lililopita – **zoezi 3.2b.** Toa kwa kila kikundi karatasi ya flipchati na kalamu.

**Pawapointi** **Somo la 3: slaidi ya 5: Maelekezo ya zoezi la 3.3**

- Waombe washiriki wazigawe karatasi zao za flipchati katika vyumba mraba vinne kama inavyoonekana kwenye slaidi na waandike maswali katika kila chumba mraba.

| **Wapo WAPI?** | **Tutumie mbinu GANI kuwabaini na kuwapata?** |
|---|---|
| **NANI katika jamii yetu anaweza kutusaidia kuwatafuta?** | **Tunaweza kukabiliwa na changamoto gani na VIPI tunaweza kuzitatua?** |

- Waeleze washiriki kwamba wazigawe karatasi zao kwa mujibu wa mfano waliopewa na wanakili vichwa vyote vya habari.
- Viombe vikundi vyote kuangalia tena kisa walichokiandika katika **zoezi la 3.2b.**
- Waombe washiriki wa kila kikundi kutafakari kuhusu kisa chao na kujibu maswali yote na kuandika majibu yao kwenye flipchati. Waambie washiriki kuwa wanaweza kuandika maneno au sentensi au wanaweza kuchora picha *(kwa mfano mandhari ya pwani pamoja na boti za uvuvi na hoteli* kuonesha mahali ambapo watoto walio nje ya skuli hupatikana*).* Fanyeni mfano mmoja pamoja kama itasaidia.
- Waombe washiriki kuchagua mtu mmoja kutoka katika kila kikundi kwa ajili ya kuripoti.
- Toa dakika 40 kwa vikundi kuandaa flipchati yao na waombe wabandike karatasi yao ukutani.
- Mtu atakayeripoti atawasilisha kazi yao mbele ya washiriki wote (toa dakika 5 kwa ajili ya kila kikundi kuwasilisha kazi yao).
- Baada ya vikundi vyote kuwasilisha kazi zao, pokea michango ya jumla. Waulize washiriki maswali yafuatayo:
    - o Iliwawia vigumu kufikiria mahali ambapo watoto walio nje ya skuli wanapatikana?
    - o Mbinu ipi katika mbinu zilizowasilishwa na vikundi itakuwa na ufanisi zaidi?
    - o Andika kwenye flipchati mbinu ambazo washiriki wanahisi zitakuwa na ufanisi zaidi na baadae zibandike juu ya ukuta. Pia ongezea pale ambapo kutakuwa na 'ukosefu' wa taarifa. Hii itakuwa ni sehemu ya zoezi la ushirikiano wa ukusanyaji taarifa baada ya kumalizika mafunzo.

## Tanbihi kwa mkufunzi

Ikihitajika, wakumbushe washiriki kuhusu **ujuzi, mikakati na nyenzo** ambazo Jumuiya za Watu wenye Ulemavu zilifanyia mazoezi na kutumia hapo kabla kama sehemu ya kujijenga uwezo wa utetezi. Hakikisha kwamba haya yanajumuishwa katika orodha ilioyopo ukutani. Nyenzo za zoeli la kukusanyia taarifa (mahojiano, makundi teule n.k.) na mtandao (kuwauliza wanafunzi kuhusu rafiki zao ambao hawaendi skuli, kuzungumza na wafanyabiashara sokoni n.k.) kutasaidia.

**Mahojiano na vikundi lengwa:** Njia nzuri ya kukusanya taarifa kutoka kwa watu katika jamii kuhusu wapi walipo watoto walio nje ya skuli na wanakabiliwa na vikwazo vipi, ni kufanya mahojiano au kuhoji vikundi lengwa. Kumbuka kwamba ni muhimu kutumia maswali ya wazi katika mahojiano na mahojiano na makundi teule, watu hujisikia faraja zaidi kuzungumzia kile wanachokijua na kufikiria. Pia kumbuka kwamba 'katika skuli' watoto wanaweza kuwa na marafiki ambao wapo nje ya skuli, kwa hivyo waulize pia.

**Ujuzi wa kusikiliza**

Ujuzi mzuri wa kusikiliza ni muhimu sana kwa ajili ya kukusanya taarifa kuhusu kile watu wanachokijua kuhusu watoto ambao wapo nje ya skuli, na wapi tutatawapata. Pia ujuzi mzuri wa kusikiliza utatusaidia kufahamu vizuri vikwazo ambavyo watoto na familia zao wanakabiliana navyo. (Tuliangalia kuhusu 'ujuzi wa kusikiliza' kama ni sehemu ya ujuzi kwa ajili ya mafunzo yanayozingatia uwezeshaji jumuishi na pia tunapoajiandaa kwa ajili ya mazoezi ya 'ukusanyaji taarifa').

**Kuchunguza kwa ajili ya utafiti**

Kuangalia kwa ajili ya utafiti ni sehemu muhimu ya hatua ya 'ANGALIA' ya duara (mzunguko) la 'ANGALIA-TAFAKARI-TENDA'. Inawezekana kuna maeneo katika jamii ambapo tunaweza kuwaangalia wanafunzi walio nje ya skuli na kuona sababu zinazowafanya wasihudhurie skuli (kwa mfano, sokoni kwa siku za skuli, - kuwaangalia wanafunzi walio nje ya skuli wakiuza mboga, wakifanya kazi uwanja wa ndege, wakipara samaki pwani, wakiwauzia vitu watalii katika au karibu na hoteli).

**Ukusanyaji taarifa katika eneo maalumu**

Ukusanyaji taarifa katika eneo maalumu kunaweza kusaidia kutambua walipo watoto walio nje ya skuli katika jamii na vikwazo wanayokabiliana nayo. Ukusanyaji taarifa katika eneo maalumu kunawezesha kupata taswira ya jamii na kujua ukubwa wa tatizo. Hii inaweza kusaidia kutafuta suluhisho na kufikiria nani katika jamii anaweza kusaidia kuwarudisha watoto hao skuli. Wakumbushe kuhusu rasilimali jamii.

# Somo la 4: Nini maana ya uhamaji katika taasisi za elimu na kwa nini ni muhimu?

### Ujumbe mahususi

- Uhamaji katika taasisi za elimu ni pale wanafunzi wanapofika skuli au kuondoka. Ni pale wanapokwenda skuli kwa mara ya kwanza, au kuhama kutoka ngazi moja, darasa au skuli moja kwenda nyengine.
- Uhamaji huwaathiri wanafunzi katika namna tofauti. Wengi hupitia nyakati za kufurahisha ijapokuwa baadhi yao hukumbana na changamoto zinazowaathiri kwa muda mrefu.
- Wakati mwengine, uhamaji katika elimu ni sehemu ya uhamaji mkubwa kwa mwanafunzi na mazingira ya uhamaji yanapaswa kufahamika vyema ili upatikane usaidizi kamili..

## Taarifa za msingi kwa mkufunzi

Uhamaji mara nyingi humaanisha watoto wanaondoka katika mazingira ya nyumbani kuelekea kwenye taasisi ya elimu na hata kwenda kwenye mazingira mapya mengine au kwenye mazingira yaleyale. Kuhama hufungua fursa mpya na changamoto kwa maendeleo ya kielimu ya mwanafunzi na makuzi. Kusimamia mchakato wa uhamaji jumuishi huwasaidia wanafunzi wote kunufaika na mabadiliko.

Uhamaji ni mchakato ambao huenda sambamba na wakati (kwa mfano) kutoka wakati ambapo watoto wanaanza kujiandaa kuanza skuli mpaka wakati ambao wameshazoea mazingira ya skuli, kinyume na wakati fulani pekee kama vile siku au wiki wanayoanza.

Uhamaji katika taasisi za elimu unaweza kuwa kipindi cha changamoto kwa wanafunzi, familia zao na walimu pia. Wanafunzi wengi huacha skuli wakati au muda mfupi baada ya kuhama, hasa ikiwa wana mahitaji maalumu ambayo hayakukidhiwa wakati wa mchakato wa uhamaji. Wakati mwengine uhamaji katika taasisi za elimu ni sehemu ya uhamaji mkubwa iwapo familia inahama kutoka makaazi yake ya kudumu kwenda kijiji chengine au kutoka kijijini kwenda mjini. Wanafunzi wanalazimika kuzoea mazingira mapya kabisa na uhamaji katika taasisi za elimu. Ni muhimu kuyatambua mabadiliko hayo ya kimazingira ili kumsaidia mwanafunzi katika kipindi hiki cha mpito.

Kwa upande wa Zanzibar skuli hupitia vipindi fulani vya kufungwa kutokana na mafuriko, magonjwa ya mripuko (mfano; Kipindupindu), mazingira machafu (mfano vyoo vibovu na vichafu) na ukosefu wa maji. Skuli pia zimefunguliwa baada ya kufungwa kufuatia ugonjwa wa UVIKO-19. Hii imepelekea wanafunzi wengi warudi skuli baada ya vipindi vya kutokuwepo. Wakati ni jambo jema kuziona skuli zikifunguliwa upya, kuna changamoto kwa wanafunzi, familia zao, skuli na walimu. Baadhi ya wanafunzi wanaingia madarasa mengine bila ya kuwaandaa kukabiliana na mazingira ya darasa jipya. Kuongezeka kwa idadi ya uandikishaji wa wanafunzi kunamaanisha uwiano wa ongezeko kubwa la wanafunzi kwa mwalimu jambo linalopelekea kuwa na madarasa yenye idadi kubwa ya wanafunzi na wanafunzi wengi wanapata wakati mgumu kushiriki kikamilifu na kufanikiwa katika mazingira hayo. Mazingira ya kujifunzia ni finyu na hili linaathiri umakini wa mwanafunzi.

### Katika somo hili washiriki:

- ü Watafahamu maana ya uhamaji katika taasisi za elimu.
- ü Watajadili jinsi gani uhamaji katika taasisi za elimu unaweza kuathiri uwepo wa mwanafunzi, ushiriki na maendeleo.

## Zoezi la 4.1: Nini maana ya uhamaji katika taasisi za elimu? Video ya uhamaji jumuishi – sehemu 1

1 dakika 30

### Maelekezo

- Tengeneza uhusiano na masomo yaliyopita kuhusu watoto walio nje ya skuli. Waulize washiriki ‘Ni hatua ipi inayofuata katika mchakato baada ya kuwatambua kwa mafanikio wanafunzi walio nje ya skuli katika eneo lako?’ Watake washiriki kujadili kuhusu ‘kuwasaidia wanafunzi kwenda au **kuhamia** skuli’.

**Pawapointi** **Somo 4: slaidi 1: Tazama video**

- Waambie washiriki kuwa wataangalia video kuhusu uhamaji wa elimu. Video hiyo imetengenezwa na EENET na inaitwa **‘Uhamaji jumuishi’.** Waombe washiriki wayatafakari maswali yafuatayo wakati wanaangalia video hiyo.

**Kuna hatua zipi tofauti za uhamaji katika taasisi za elimu?**

**Kwa nini uhamaji katika taasisi za elimu ni muhimu?**

- Tazama filamu: https://www.youtube.com/watch?v=X1Ul_5wrsAE . Sitisha filamu itakapofika katika **dakika ya 3.06.** Maelezo ya video yanapatikana katika **Kielelezo nam. 5.1.**
- Baada ya kuangalia video, katika majadiliano waombe washiriki wakupatie mrejesho kuhusu maswali mawili uliyowauliza. Usitegemee majibu ya maana sana kwa swali la pili katika hatua hii kwa kuwa swali hili litaangaliwa kwa kina baadae.
- Waoneshe maana ifuatayo ya uhamaji katika taasisi za elimu ambayo imeandikwa kwenye flipchati na/au kwenye slaidi ya PawaPointi na isome kwa sauti. Karibisha michango au maswali.

**Power Point** **Somo la 4: slaidi ya 2: nini maana ya uhamaji katika taasisi za elimu?**

**Uhamaji katika taasisi za elimu** hutokea pale wanafunzi wanapowasili au kuondoka skuli, ni pale watoto wanapokwenda skuli kwa mara ya kwanza, au kuhama kutoka ngazi, darasa au skuli moja kwenda nyengine. *Kwa mfano kujiunga na skuli ya maandalizi, kuhama kutoka darasa la tano kwenda la sita au kuondoka skuli ya msingi na kujiunga na sekondari au kutoka sekondari kwenda chuoni.*

"Uhamaji ni mchakato ambao huenda sambamba na wakati (kwa mfano) kutoka wakati ambapo watoto wanaanza kujiandaa kuanza skuli mpaka wakati ambao wameshazoea mazingira ya skuli, kinyume na wakati fulani pekee kama vile siku au wiki wanayoanza. "

Uhamaji katika taasisi za elimu unaweza kuwa kipindi cha changamoto kwa wanafunzi, familia zao na walimu pia. Wanafunzi wengi huacha skuli wakati au muda mfupi baada ya kuhama, hasa ikiwa wana mahitaji maalumu ambayo hayakukidhiwa wakati wa mchakato wa uhamaji.

## Zoezi la 4.2: Uzoefu wetu wenyewe katika uhamaji katika muktadha wa kielimu

1 dakika 45

### Maelekezo

- Waombe washiriki kutafakari kuhusu uzoefu wao wenyewe wa uhamaji wa elimu. Waombe washiriki wakae wawiliwawili wakijaribu kukumbuka **kilichowatokea** na **walijisikiaje** kama wanafunzi walipojiunga na skuli nyengine au walipolazimika kubadili darasa/skuli katikati ya muhula. Mkufunzi anaweza kujielezea yeye mwenyewe kama mfano ili kuwahamasisha washiriki watafakari na kusimulia.

**Pawapointi** **Somo la 4: slaidi ya 3-4: Maelekezo kuhusu zoezi 4.2**

- Baada ya dakika 10-15, waombe wa shiriki walio tayari kujitolea kutoa mrejesho kwa mbele ya washiriki wote, mrejesho chanya mmoja na hasi mmoja ambao ulisimuliwa na mwanakikundi.
- Baadae waombe washiriki waendelee kushirikiana katika jozi na kujadili yafuatayo:
  - **Aina gani ya kipindi cha mpito (uhamaji) ambacho wanafunzi katika wilaya/ eneo lako wanakipitia?**

    (Mkufunzi anaweza kutoa baadhi ya mifano kama vile: Kutoka nyumbani kwenda katika mazingira ya elimu ya maandalizi/msingi, msingi kwenda sekondari, sekondari kwenda elimu ya juu; Mwanafunzi mwenye ulemavu kutoka skuli maalumu kwenda katika skuli ya kawaida au kinyume chake; Kurudi skuli baada ya kutohudhuria kwa muda (kwa mfano kwa sababu ya ugonjwa au uhamaji wa ndani kwenda kjiji chengine au eneo jengine); Kufika skuli katikati ya muhula (kutokana na ukimbizi wa ndani).
  - **Iwapo baadhi ya wanafunzi wanafika au kuondoka nje ya muda uliopangwa, kwa nini wanafanya hivyo?**
  - **Je! Wanafunzi wanaohama (walio kwenye kipindi cha mpito) wanasaidiwa? Wanasaidiwaje?**
- Mwisho, waombe washiriki watoe mrejesho wa walichofikiria mbele ya washiriki wote, na nakili mawazo yao kwenye ubao au flipchati.

## Zoezi la 4.3: Kwa namna gani uhamaji katika taasisi za elimu huwaathiri wanafunzi?

1 dakika 30

Lengo la zoezi hili ni kuwasaidia washiriki kufahamu ni kwa namna gani uhamaji wa kielimu unaweza kuathiri mchakato wa kujifunza.

### Maelekezo

- Katika vikundi, waambie washiriki kwamba wataangalia baadhi ya mambo ambayo wanafunzi waliyasema walipokuwa wanahama kutoka katika mazingira ya awali kwenda katika mazingira mengine.
- Wapatie nakla ya **Kielelezo nam. 4.3: walichokisema wanafunzi** kwa kila kikundi na waombe wajadili nukuu. Waombe wajadili maswali mawili yafuatayo katika vikundi vyao:
    1. **Unakumbuka hisia kama hizo na hali waliyopitia wanafunzi? (Rejea zoezi 4.2).**
    2. **Unadhani kwa namna gani uhamaji uliathiri hali aliyokuwa anapitia mwanafunzi skuli na kujifunza?**
    3. **Inamaanisha nini kwao wanapohama?**

**Pawapointi** **Somo la 4: slaidi ya 5: Maelekezo kwa ajili ya zoezi la 4.3**

- Katika mjadala pokea mrejesho kutoka kwa washiriki na nakili majibu yao kwa ajili ya swali la pili kwenye flipchati (hakuna haja ya kunakili majibu ya swali nambari 1).

# Somo la 5: Uhamaji jumuishi unaanzia nyumbani

## Ujumbe mahususi

- Wazazi na familia ndio walimu wa mwanzo wa mtoto. Familia, nyumbani na jamii zinabaki kuwa taasisi muhimu kadiri mtoto anavyopitia ngazi mbalimbali za elimu.
- Kujiunga na elimu ya maandalizi na skuli haimaanishi kuwa ndio mwisho wa kujifunza katika mazingira ya nyumbani. Ili iwe rahisi kuhamia katika mazingira ya elimu jumuishi, ni muhimu kuwahusisha wazazi.
- Mambo yanayohusiana na maisha ya mtoto ya nyumbani ambayo huathiri mahudhurio au ushiriki wake katika elimu anapoondoka kutoka nyumbani kwenda skuli kila siku.

## Taarifa za msingi kwa ajili ya mkufunzi

Kuanzia wakati mtoto anapozaliwa, anakabiliana na mabadiliko; kukua na kujifunza vitu vipya, kukutana na watu wapya na kupitia mazingira mapya. Mazingira ya awali ya kujifunza na makuzi ambayo watoto hupitia ni katika familia zao, nyumbani na katika jamii. Wakati watoto wanahama kutoka katika ngazi moja kwenda nyengine katika mfumo rasmi wa elimu, familia zao, nyumbani na jamii zinabaki kuwa taasisi muhimu muda wote.

Wazazi na familia mara nyingi ndio watetezi wa mwanzo wa elimu mjumuisho wakati wa uhamaji. Wanaweza kuchagua taasisi ya elimu, kuendesha utetezi unaolenga kuhakikisha mazingira mapya ya elimu yanatambua na kukidhi mahitaji ya mtoto wao, kuhakikisha kwamba mtoto wao ana nyenzo zote anazozihitaji ili ajumuishwe kikamilifu, na kumuandaa mtoto wao kwa ajili ya mabadiliko. Pia wana ujuzi wa kutosha kutambua aina ya msaada mtoto wao anaouhitaji.

Skuli na walimu wanaoratibu uhamaji wawawezeshe wazazi na familia kuongoza mchakato wakitaka, na/au kuwashauri katika kila hatua inayoendelea.

Kinachomtokea mtoto kila siku kabla ya kuondoka kwenda skuli kinaweza pia kuathiri safari yake ya kwenda skuli na siku yake nzima. Baadhi ya mambo muhimu tunayopaswa kuyazingatia ni pamoja na: usingizi, kifungua kinywa na majukumu ya nyumbani.

- Uchovu unaathiri kujifunza na ustawi.

- Njaa inaathiri umakini na afya.
- Majukumu ya nyumbani yanaweza kuwa sehemu ya kujifunza ujuzi na majukumu, lakini pia yanaweza kuathiri uwezo wa mtoto kujifunza iwapo atachoka, atachafuka au kuchelewa skuli.

### Katika somo hili washiriki:

ü Watatafakari kuhusu umuhimu wa wazazi na familia katika uhamaji katika taasisi za elimu
ü Kuangalia mambo yanayoathiri safari ya mwanafunzi kwenda skuli kila siku
ü Kutafuta njia za kuondoa wasiwasi wa wazazi na kuwahamasisha kushiriki katika kusaidia mchakato wa safari ya mwanafunzi.

## Zoezi la 5.1: Kujifunza na makuzi nyumbani

Zoezi hili linasaidia kuwaandaa washiriki kutafakari kuhusu uhamaji jumuishi kwa kuangalia mazingira tofauti ya kujifunza, makuzi na elimu na safari wanayopitia watoto wakati wanapokwenda skuli.

## 5.1a: Mazingira ya elimu

1 dakika 30

**Pawapointi** **Somo la 5: slaidi ya 1: Maelekezo kwa ajili ya zoezi la 5.1a**

### Maelekezo

- Wagawe washiriki katika vikundi vipya vya watu 4-5. Wape flipchati na kalamu au penseli za rangi. Wape washiriki maelekezo yafuatayo:

  ü Chora picha tatu tofauti: ya kwanza inayoonesha mazingira ya nyumbani, ya pili inayoonesha malezi ya utotoni na nyengine mazingira ya elimu, na moja ya mazingira ya skuli

  ü Katika picha yako ingiza mambo yafuatayo:

  –Watu

  –Jinsi wanavyohusiana

  –Shughuli wanazofanya

–Jinsi ya eneo lilivyopangiliwa (kwa mfano mazingira ya chumbani)

–Samani, vifaa na vitu vyengine (kwa mfano meza, saa, miti)

ü Michoro inaweza kuwa ya kawaida tu, ikijumuisha katuni za watu au alama, au yenye taarifa zaidi ukitaka. Andika majina au maelezo mafupi ili kuwasaidia watu wengine wafahamu mchoro wako. Una dakika 20 kukamilisha zoezi hili.

**Tanbihi kwa mkufunzi**

Andaa somo lako kwa mujibu wa eneo walipo washiriki wako; unaweza kujumuisha taasisi nyengine za elimu ambazo wanafunzi wanahudhuria katika wilaya yao kama vile skuli ya sekondari au Chuo Kikuu. Ni muhimu kusisitiza kwamba hii si sehemu ya maandalizi ya mafunzo, bali ni namna ya kutafakari kwa kuzingatia ushirikishi, shughuli, eneo na rasilimali zinazopatikana katika taasisi hizi.

- Baada ya dakika 20, waombe washiriki katika vikundi vyao kuongeza wastani wa umri wa watoto katika kila taasisi kwa kuzingatia mfumo wa elimu katika eneo lao.
- Waambie washiriki kubandika picha zao tatu ukutani na wazipange katika namna itakayoonesha uhusiano baina yao.

## 5.1b: Video ya uhamaji jumuishi – Sehemu ya pili

1 dakika 30

### Maelekezo

- Waambie washiriki kwamba watatazama sehemu ya pili ya video fupi ya **'uhamaji jumuishi'** ilioandaliwa na EENET.
- Tazama video: https://www.youtube.com/watch?v=X1UI_5wrsAE **dakika** ya 3.06 mpaka 5.35. Maelezo ya video hiyo yanapatikana katika **Kielelezo nam. 4.1.**

**Pawapointi** **Somo la 5: slaidi ya 2: Maelekezo kwa ajili ya zoezi la 5.1b**

- Waombe washiriki kufanya kazi pamoja katika vikundi vilevile kama awali na watafakari kwa namna gani familia:

1. **Zinasaidia mchakato wa watoto kujifunza katika siku za awali na makuzi nyumbani.**
2. **Zinaendelea kusaidia mchakato wa watoto kujifunza na makuzi wanapojiunga na skuli za maandalizi**
3. **Zinaendelea kusaidia watoto kujifunza na makuzi wanapoingia skuli za msingi au sekondari**

- Haya yanaweza kuwa mambo ambayo waliyaona katika filamu au kutokana na uzoefu wao wenyewe. Washiriki katika vikundi wachague mifano mitatu watakayoiandika katika bango lao na kubandika katika picha yao ya **mazingira ya elimu** iliyopo ukutani.
- Waambie washiriki sasa wazunguke kuangalia picha za vikundi vyengine za **mazingira ya elimu** na mifano myengine ambayo vikundi vyengine waliitoa.
- Katika majadiliano uliza maswali yafuatayo:
  - Kipi kinafanana na kipi ni tofauti katika michoro hii?
  - Picha hizi tatu zimepangiliwa vipi, zimepangiliwa katika mstari mmoja au zimepangiliwa wima au katika mpangilio mwengine?
  - Je! mifano iliyotolewa inalingana au ni tofauti na mifano ya vikundi vyengine?
  - Je! Ilikuwa vigumu kufikiria mambo matatu amabayo familia huyafanya kila siku ili kusaidia mchakato wa mtoto kujifunza katika kila ngazi ya elimu?

## Zoezi la 5.2: Jukumu la familia katika uhamaji

Lengo kuu la zoezi hili ni kutambua:

a) Uhusikaji wa familia katika elimu ya mtoto wao/uhamaji

b) Wasiwasi na hisia ambazo wazazi na familia wanao kuhusu uhamaji wa mtoto wao

c) Mikakati kwa ajili ya kuondoa wasiwasi wa wazazi na kuhamasisha ushiriki wao katika mchakato wa uhamaji.

## 5.2a: Ushiriki wa familia katika mchakato wa uhamaji katika taasisi za elimu

1 dakika 20

**Pawapointi** **Somo la 5: slaidi ya 3-5: Jukumu la familia katika mchakato wa uhamaji katika taasisi za elimu**

### Maelekezo

- Wasilisha yafuatayo (katika slaidi 3):

| |
|---|
| **Wazazi na familia** ni sehemu muhimu katika elimu ya mtoto. Famila, nyumbani na jamii inabaki kuwa nguzo muhimu kadiri mtoto anapohama kwenda katika ngazi tofauti za elimu.<br><br>Kuanza kwenda skuli hakumaanishi kuwa ni mwisho wa mtoto kujifunza nyumbani. Ili kuhakikisha kwamba uhamaji huu hauna vikwazo na jumuishi ni muhimu kuwahusisha wazazi na walezi. |

- Onesha mchoro kwenye slaidi ya 4 na waulize washiriki wanaona nini katika picha. Vyenginevyo unaweza kuwapa picha kama kitini kwenye **Kielelezo nam. 5.2a.**
- Waombe washiriki waendelee na zoezi katika vikundi vilevile kama ilivyokuwa kwa zoezi lililopita.
- Onesha maelekezo kwa zoezi la 5.2a kwenye slaidi ya 5. Muombe mshiriki mmoja kutoka katika kila kikundi kwenda kuuangalia vizuri mchoro wa mazingira ya elimu. **Je! Wazazi na familia zinaonekana katika mazingira yote?**
- Katika vikundi vyao wajadili **kwa nini zinaonekana, au hazionekani.** Vikundi vitengeneze orodha ya ushirikishwaji wa wazazi na familia katika kila mazingira ya elimu kwa mujibu wa uzoefu wao. Tumia maswali yafuatayo kama muongozo ikihitajika:
  - ü **Ni mara ngapi wazazi au familia huonekana katika taasisi za elimu? Wanakuja kufanya nini?**
  - ü **Je! Wazazi hushirikishwa katika ufanyaji wa maamuzi? Je! Wana sauti katika kile kinachofanyika katika taasisi za elimu? Kama wanayo, ni kwa namna gani?**

ü **Je walimu wanawasiliana vipi na wazazi na familia zao?**

ü **Ni yepi majukumu/matarajio ya wazazi na familia?**

- Anzisha mjadala mdogo, ukikaribisha mawazo machache kutoka katika kila kikundi.

**Pawapointi** Somo la 5: slaidi ya 6

- Wasomee nukuu ifuatayo:

  "Wazazi na familia mara nyingi ndio watetezi wa awali wa elimu ya mtoto wao. Huchagua skuli, wakiiomba skuli kutambua na kukidhi mahitaji ya mtoto wao, kuhakikisha kwamba mtoto wao ana nyenzo zote zinazohitajika ili aweze kujumuishwa kikamilifu, na kumuandaa mtoto wao kwa ajili ya mabadiliko. Wao pia ndio wenye kujua kuhusu mahitaji ya msaada ya mtoto wao. Haya yote ni majukumu muhimu ambayo wazazi na familia huyatekeleza wakati wa uhamaji katika taasisi za elimu."

## 5.2b: Wasiwasi wa wazazi kuhusu uhamaji wa mtoto wao

1 dakika 20

### Maelekezo

- Wape washiriki wa kila kikundi karatasi isiyo na maandishi ya A4 na waombe washiriki kuvipitia visa mkasa viwili kutoka kwenye **Zoezi la 3.2. Visa mafunzo kuhusu watoto walio nje ya skuli.**
- Waombe washiriki katika kila karatasi waliopewa (moja kwa kila kisa), kuandika 'familia ya [Andika jina la mtoto aliyetajwa katika kisa ]'. Wanaweza pia kuchora picha ya mtoto katikati.

**Pawapointi** **Somo la 5: slaidi ya 7**

- Waambie washiriki kuvaa uhusika wa familia ya mtoto. Jaza nafasi iliyobakia kwenye karatasi na **maneno na maelezo yanayoelezea hisia, hali ya huzuni au furaha na wasiwasi ambao wazazi na wanafamilia ya mtoto huyu watakuwa nao wanapopanga safari ya kumpeleka mtoto wao katika mazingira mapya ya elimu, skuli au kituo cha maandalizi.**

- Waoneshe zoezi kwenye karatasi au flipchati na toa mfano mmoja au miwili ya hisia za wazazi ‘hisia au wasiwasi’ ili kuwahamasisha waanze (angalia kwenye kisanduku cha ‘tanbihi kwa mkufunzi’).
- Baada ya dakika 10, pokea mrejesho mfupi kutoka kwa vikundi vichache. Zingatia maneno au maelezo ambayo yamejitokeza sana katika visa mkasa vingi na yale ambayo ni ya kipekee.

**Tanbihi kwa mkufunzi:**

Majibu yanapaswa kuwa tofauti kwa kikla kikundi kwa kutegemea kisa mkasa maalumu walichopewa. Aina ya majibu yanaweza kujumuisha:

- Hawajui kuwa mtoto wao anaruhusiwa kwenda skuli.
- Wanajua kwamba hakuna mtu anayemjua zaidi mtoto wao kuliko wao wanavyomjua.
- Hawajui mfumo wa elimu ulivyo.
- Wanatamani kumlinda mtoto wao au kumuweka mbali na jamii.
- Wanaona aibu.
- Wanaamini sehemu nzuri kwa mtoto wao ni nyumbani.
- Hawafikirii kwamba mtoto wao atanufaika na elimu ya skuli.
- Wanadhani mtoto wao hatoweza kujifunza
- Wanadhani mtoto wao hatoweza kujifunza kwa kasi saw ana watoto wengine.
- Mtoto wao anazungumza lugha tofauti kwa hivyo wanadhani hakuna skuli inayomfaa.
- Hawajui kwamba na wao wana haki ya kupata elimu katika jamii hii.
- Wana hofu.
- Hawamjui mtu yeyote katika jamii hii.
- Hawamudu gharama za kumuandikisha mtoto wao skuli
- Wana kumbukumbu za madhara yaliyowahi kuwapata katika elimu.
- Wao hawajasoma kwa hivyo wana hofu huenda wasiweze kumsaidia mtoto wao kujifunza.

## 5.2c: Mbinu za kushughulikia maoni ya wazazi na kuhamasisha ushiriki wao katika mchakato wa uhamaji.

1 dakika 20

**Pawapointi** **Somo la 5: slaidi ya 8: mbinu za kushughulikia wasiwasi wa wazazi kuhusu uhamaji katika taasisi za elimu**

### Maelekezo

- Waambie washiriki kwamba kuna mbinu tofauti zinazoweza kusaidia kushughulikia wasiwasi wa wazazi na familia kuhusu uhamaji katika taasisi za elimu na kuwahamasisha kushiriki ipasavyo katika kufanikisha mchakato wa uhamaji.
- Gawa seti moja ya picha tatu kutoka kwenye **Kielelezo nam. 5.2b: (picha tatu) mbinu za kushughulikia wasiwasi wa wazazi kuhusu uhamaji katika taasisi za elimu** kwa kila kikundi. Waombe washiriki katika vikundi kuziangalia picha na kujadili swali:
  - ü **Mbinu gani ya kusaidia uhamaji katika taasisi za elimu ambayo imeoneshwa katika picha?**
- Pokea mrejesho mfupi halafu eleza mbinu zilizooneshwa katika picha:
  1. Walimu **wanatembelea** nyumbani kwa wanafunzi
  2. Kuandaa na kusambaza **vipeperushi vya kutoa elimu, usaidizi na kujenga uelewa kuhusu elimu** kwa wazazi na familia
  3. Kuandaa **siku maalumu ya kuruhusu watu kutembelea skuli au siku ya uandikishaji wa wanafunzi wapya** (kuzialika familia kutembelea skuli)
- Waombe washiriki katika vikundi vyao kujadili yafuatayo:
  - ü **Kwa namna gani kila mbinu itasaidia kuondosha wasiwasi wa wazazi na kuwahamasisha kushiriki ipasavyo katika mchakato wa uhamaji? (Fikiria visa mkasa ambavyo ulivisoma hapo kabla)**
  - ü **Mbinu gani nyengine ambazo ungepenedekeza ili kusaidia kuondosha wasiwasi wa wazazi na kuwahamasisha kushiriki kikamilifu katika mchakato wa uhamaji?**
- Wahamasishe washiriki kufikiria kuhusu visa mkasa ambavyo waliviangalia hapo kabla na kwa namna gani mbinu hizi zingeweza kusaidia katika kila kisa.

**Pawapointi** **Somo la 5: slaidi ya 9-11: mbinu (picha 3)**

- Katika mjadala waombe washiriki kutoka katika baadhi ya vikundi kutoa mawazo yao. Onesha picha tatu za kwenye slaidi kusaidia mjadala. Waulize washiriki katika vikundi vyengine iwapo wana mifano myengine ya zoezi kama hilo ili kusaidia uhamaji katika skuli ndani ya wilaya zao. Waulize:
  - ü **Kuna jitihada zozote zilizochukuliwa kuwasaidia wanafunzi warudi skuli baada ya kutohudhuria au skuli kufungwa?**

**Pawapointi** **Somo la 5: slaidi ya 12: Umuhimu wa ushiriki wa familia katika mchakato wa uhamaji katika taasisi za elimu**

- Mwisho, waeleze yafuatayo:

  "Watoto na familia zao wanapohusishwa katika mchakato wa kuhama, kuna uwezekano mkubwa wa kupatikana mafanikio. Ikiwa familia hazishiriki ipasavyo, zitahitaji kuhamasishwa na kusaidiwa na walimu, kamati ya ujumuishi ya skuli, na Jumuiya za Watu wenye Ulemavu. Hii ni muhimu hasa kwa watoto walio katika mazingira magumu. Tunapaswa kuhakikisha kwamba watoto wote, bila ya kujali historia yao, wanasaidiwa kurudi skuli katika mfumo wa elimu jumuishi."

## Zoezi la 5.3: Changamoto zinazowakabili wanafunzi kabla ya kwenda skuli - filamu

Lengo kuu la zoezi hili ni kuwahamasisha washiriki kufikiria baadhi ya sababu ambazo chanzo chake ni maisha ya nyumbani ambazo zinaathiri mahudhurio yao au ushiriki wao katika elimu, na kwa jinsi gani zinaweza kupunguza athari hasi.

1 dakika 45

### Maelekezo

- Wagawe washiriki katika vikundi vitatu. Kila kikundi kitashughulika na sababu tofauti ambayo inaweza kuathiri mahudhurio ya mwanafunzi au ushiriki katika elimu wanapopitia katika mchakato wa kwenda skuli kila siku.

**Pawapointi** **Somo 5: slaidi 13-14**

- Sisitiza kwamba zinaweza kuwepo sababu nyengine muhimu ambazo pia huathiri mchakato wa mwanafunzi kwenda skuli kila siku. Sababu hizo ikiwemo kufanyiwa fujo wakati anapokwenda skuli, kwa mfano, ambayo inaweza kumjengea hofu na kuzuia uwepo au ushiriki wake. Hata hivyo zoezi hili linalenga usingizi (kulala), kifungua kinywa na majukumu ya nyumbani.
- Kikundi cha kwanza kitaangalia **usingizi (kulala),** kikundi cha pili **kifungua kinywa** na kikundi cha tatu **majukumu ya nyumbani.** Wapatie maelezo sahihi kutoka katika **Kielelezo nam. 5.3a** (angalia visanduku vilivyopo hapa chini).

**Kikundi cha 1, fikiria kuhusu usingizi**

Chukua kipande cha karatasi ya flipchati na chora mchoro wa mtoto aliyelala katikati. Baadae jadilini yafuatayo na andikeni maelezo kwenye flipchati:

- Mambo gani katika jamii yako ambayo husababisha watoto katika jamii yako wasipate usingizi wa kutosha?
- Kwa namna gani ukosefu wa usingizi huathiri ujumuishwaji wa watoto katika elimu?
- Kwa namna gani usingizi husaidia ujumuishwaji wa watoto katika elimu?
- **Nini kifanyike** ili kuhakikisha watoto wanapata usingizi wa kutosha?

**Kikundi cha 2, fikiria kuhusu kifungua kinywa.**

Chukua kipande cha karatasi ya flipchati na chora mchoro wa mtoto anayepata kifungua kinywa katikati, au hata picha ya bakuli na kijiko. Baadae jadili yafuatayo na andika maelezo kwenye flipchati:

- Kwa nini inawezekana watoto katika jamii yako wasipate kifungua kinywa kabla ya kwenda skuli?
- Kwa namna gani ukosefu wa kifungua kinywa huathiri ujumuishwaji wa mtoto katika elimu?
- Kwa namna gani upatikanaji wa kifungua kinywa husaidia ujumuishwaji wa watoto katika elimu?
- **Nini kifanyike** ili kuhakikisha watoto wanapata chakula kabla hawajatoka kwenda skuli?

**Kikundi cha 3 watafikiria kuhusu majukumu ya nyumbani.**

Chukua kipande cha karatasi ya flipchati na chora mchoro wa mtoto akifanya kazi za nyumbani. Baadaye jadilini yafuatayo na andikeni maelezo kwenye flipchati:

- Kazi zipi ambazo watoto katika jamii yako huzifanya na kwa nini hufanya kazi hizo?
- Kwa namna gani kazi za nyumbani, shambani au katika jamii huathiri uwezo wa mtoto kujifunza?
- Kwa namna gani kazi hizo zinaweza kumsaidia mtoto kujifunza?
- **Nini kifanyike** ili kuhakikisha kazi hizo haziathiri ujumuishwaji wa mtoto katika elimu?

- Washiriki wote katika vikundi watafakari kuhusu uzoefu walioupata walipokuwa wadogo, na pia watoto wanaowajua. Waombe watoe mifano ili kufafanua hoja zao.
- Baada ya dakika 15, sitisha zoezi lakini usipokee mrejesho kwanza. Waambie washiriki kwamba hivi sasa tutaangalia video nyengine iliyoandaliwa na EENET kutoka katika mfululizo wa 'Siku Jumuishi' inayoitwa **'Kabla ya kwenda skuli'.** (Video hii ipo katika *flashi diski* walizopewa wakati wa mafunzo ya moduli ya msingi na ni ya kwanza katika mfululizo wa filamu 10 kuhusu siku jumuishi ya skuli).
- Waombe washiriki wakati wanatazama filamu kufikiria iwapo wana chochote ambacho wangependa kuongezea katika flipchati ya kikundi chao 'usingizi', 'kifungua kinywa', na 'majukumu'.
- Tazama video kuanzia mwanzo mpaka mwisho, ina urefu wa dakika 7.30. https://www.youtube.com/watch?v=fhi1PiMoYLc . Maelezo ya filamu yanapatikana katika **Kielelezo nam. 5.3b.**
- Baada ya kutazama filamu wape washiriki dakika 10 nyengine za kujadili walichokiona katika filamu na watafakari iwapo kuna chochote chengine ambacho wangependa kuongezea katika flipchati yao.
- Mwisho waalike washiriki kutoka katika kila kikundi kubandika flipchati yao ukutani.
- Mwanakikundi mmoja kutoka katika kila kikundi asimame kando ya flipchati yao. Washiriki wengine kutoka katika kikundi watatembelea flipchati nyengine kuangalia kilichojadiliwa. Wanaweza kuongeza hoja zaidi katika flipchati wakihisi kuna hoja iliyoachwa. Vyenginevyo unaweza kulifanya

zoezi hili kama ziara ya makumbusho ambapo washiriki wanazunguka kwenye ukumbi na kusoma flipchati za vikundi vyengine.

- Tumia dakika 5-10 katika kila flipchati na baadae nenda katika flipchati nyengine.

## Tanbihi kwa mkufunzi

Unaweza kutumia mawazo haya kujaza mapengo katika majibu ya washiriki, au kuwasaidia ukihisi wanapata tabu ya kufikiria majibu.

### Usingizi

**Kwa nini unadhani watoto hawapati usingizi wa kutosha?**

- Kelele, usumbufu, kazi nyingi, kazi nyingi za nyumbani, kuumwa, huzuni, furaha.
- Kuangalia michezo au filamu, kutumia mitandao ya kijamii usiku wa manane.

**Ukosefu wa usingizi huathiri ujumuishwaji wa watoto katika namna tofauti kama vile:**

- Kukosa umakini, kukosa kumbukumbu, kukosa furaha, kulala darasani, uchovu, kutopenda kuchanganyika na wenzao, kuwa mkali.

**Nini kifanyike ili kuhakikisha kwamba watoto wanapata usingizi wa kutosha ili waweze kujifunza kwa ufanisi?**

- Watafute watoto waliochoka na wanaolala darasani (Kwa mfano kupitia Kamati ya Elimu Mjumuisho ya Skuli). Zungumza na wazazi wao kutafuta chanzo.
- Washauri wazazi kuhusu umuhimu wa usingizi. Au zihamasishe zahanati jirani au wafanyakazi wa jamii kuendesha kampeni ya afya na ustawi kuhusu umuhimu wa watoto kupata usingizi wa kutosha.

### Kifungua kinywa

**Kwa nini watoto hawapati kifungua kinywa kabla ya kwenda skuli?**

- Familia haimudu kifungua kinywa, wazazi hawana muda wa kuwaandalia, au wanakuwa wameshatoka kwenda kazini mapema asubuhi, muda ni mfupi mno – kwa mfano kwa sababu wanafanya kazi za nyumbani au wanalazimika kutembea masafa marefu kwenda skuli, au wanachelewa kuamka asubuhi.

**Kutopata kifungua kinywa huathiri ujumuishwaji wa watoto katika elimu**

- Kukosa umakini na kushindwa kuwa na kumbukumbu, kuwa na hasira na

huzuni, wasiwasi, msongo wa mawazo, kuwa mbali kifikra, kuwa na tabia mbaya skuli.

- Kushindwa kushiriki ipasavyo katika masomo au kazi za vitendo, kama vile michezo.
- Udumavu katika makuzi ya kimwili na kiakili.
- Kushindwa kuhudhuria skuli jambo linaloweza kupelekea kushindwa kuendelea na masomo au kufeli mitihani.

**Nini kifanyike ili kuhakikisha watoto wanakula kabla ya kwenda skuli?**

- Fanya uchunguzi ili kuwatambua watoto wenye njaa. Zungumza na watoto na wazazi ili kujua kwa nini wanakuja skuli na njaa. Elezea umuhimu wa kupata kifungua kinywa katika kumuwezesha mtoto kujifunza na wanasihi wazazi kuwapatia watoto wao kifungua kinywa ikiwezekana.
- Wasiliana na kituo cha huduma za afya au ustawi kujua iwapo kuna msaada wowote kwa ajili ya familia ambazo hazimudu kuwaandalia watoto wao kifungua kinywa.
- Shirikiana na skuli/kamati ya elimu mjumuisho ya skuli kuanzisha klabu za kifungua kinywa, ikiwezekana kwa msaada wa wanajamii au wafanyabiashara wa eneo hilo.
- Wasiliana na jumuiya ambazo zinaweza kuwasaidia wazazi kujiongezea kipato ili waweze kuwapatia watoto wao chakula ipasavyo.
- Programu ya utowaji wa chakula katika skuli inayofadhiliwa na WFP au UNICEF.

## Majukumu

**Watoto hufanya kazi gani?**

- Kazi za nyumbani kama vile usafi, kupika, kuchota maji na kutafuta kuni; kuwahudumia wadogo zao, wazee au ndugu wenye ulemavu; kuhudumia mifugo; kuuza bidhaa sokoni au mtaani; kupanda, kupalilia na kuvuna mazao.

**Kwa nini majukumu yanaweza kuathiri ujumuishwaji wa watoto katika elimu?**

- Watoto wanaweza kuwa wamechoka kiasi cha kushindwa kusoma au kuja skuli kabisa.
- Wanaweza kuchelewa kufika skuli, kukosa vipindi au kuadhibiwa kwa

kuchelewa.

- Wanaweza kufika skuli wakiwa wachafu na kuadhibiwa.
- Watoto wanaweza kuhisi wanafaidika zaidi na kazi zinazowapatia pesa kuliko kuja skuli na wanaweza kuamua kuacha kabla ya kumaliza.

**Kwa namna gani kazi huchangia kujifunza?**

- Watoto wanaweza kujifunza ujuzi, uwezo wa kuchambua na kutatua changamoto – ujuzi ambao ni muhimu katika maisha yao na huwasaidia pia katika masomo yao.
- Kumjengea mtoto tabia ya kujali kuwajibika, kujiamini na bidi.
- Baadhi ya kazi huisaidia familia kujiongezea kipato ambacho kinaiwezesha familia kumudu gharama za kusomesha watoto.
- Watoto hujifunza ujuzi wa kupanga na kuratibu mambo.

**Nini kifanyike ili kuhakikisha kwamba majukumu hayaathiri ujumuishwaji wa watoto katika elimu?**

- Unaweza kuzungumza na watoto na wazazi wao ili kujua kazi wanazozifanya, hasa ukiwa na wasiwasi kwamba mtoto anaathirika na majukumu aliyopewa.
- Mshauri mzazi kupunguza au kurekebisha ratiba ya kazi za mtoto kupunguza athari inayoweza kujitokeza katika uhudhuriaji wa mtoto skuli.
- Waombe walimu kurekebisha kanuni zao, ili masomo yachelewe kuanza au watoto wanaofanya kazi asubuhi wasiadhibiwe kwa uchelewaji.
- Wasiliana na jumuiya za eneo hilo ambazo zinaweza kuwasaidia wazazi kuongeza kipato chao ili wasitegemee kazi zinazofanywa na mtoto wao.

· Katika majadiliano pokea mrejesho mfupi kutoka katika kila kikundi kuhusu mbinu zinazoweza kutumika kushughulikia changamoto hizo tatu. Mbinu hizo zijikite katika ushauri unaojibu swali 'nini kifanyike ……' swali.

· Onesha slaidi ya PPT yenye mchoro wa programu ya utowaji wa kifungua kinywa skuli na uliza ni washiriki wangapi wanatambua uwepo wa programu kama hiyo katika wilaya zao.

**Pawapointi**

**Somo la 5: Slaidi ya 15: programu ya kifungua kinywa skuli**

# Somo la 6: Jukumu la Jumuiya za Watu wenye Ulemavu katika kuwatambua wanafunzi walio nje ya skuli na kusaidia uhamaji jumuishi

**Ujumbe mahususi**

- Uhamaji jumuishi huanzia nyumbani na katika jamii na huendelea katika safari ya kuelekea skuli, mwanafunzi anapowasili skuli na pia darasani. Kusaidia uhamaji jumuishi ni wajibu wa wazazi na walezi na pia wafanyakazi wa skuli na walimu.
- Jumuiya ya watu wenye ulemavu ina jukumu la msingi katika kuwatambua wanafunzi walio nje ya skuli lakini pia katika kuwezesha uhamaji jumuishi. Jukumu hili linaweza kutekelezwa katika sura tofauti, ikiwemo:
  - na kukusanya taarifa za hoja za kuleta mabadiliko
  - Kuwezesha ushirikiano ili kujenga umoja thabiti na mtandao kwa ajili ya kuleta mabadiliko
  - Kukuza uwelewa kuhusu mabadiliko yanayohitajika kwa ajili ya elimu jumuishi
  - Kutumia sera kushawishi ufanyaji wa maamuzi kwa ajili ya mabadiliko
  - Kufuatilia na kusaidia mchakato wa mabadiliko kwa ajili ya elimu jumuishi

## Taarifa za msingi kwa ajili ya mkufunzi

Somo hili linaangalia mbinu tofauti ili kusaidia uhamaji jumuishi. Linaangalia mbinu tofauti ambazo aidha zitakuwa ni jukumu la skuli au kamati ya elimu mjumuisho ya skuli (SIT), na pia mikakati ambayo inaweza kuanzishwa na/au kuwezeshwa na jumuiya za kijamii zikiwemo Jumuiya za Watu wenye Ulemavu.

Kwa kuongezea, somo hili linakaribisha mjadala kuhusu fursa kwa ajili ya kushirikiana katika kuwatambua wanafunzi walio nje ya skuli na kusaidia uhamaji jumuishi katika ngazi zote. Zoezi la mwisho linakaribisha skuli za majaribio kuelezea walitumia mbinu zipi kuwatambua watoto walio nje ya skuli na kusaidia uhamaji jumuishi. Katika ngazi ya taifa muhutasari wa mbinu/mikakati inayotekelezwa na kamati ya elimu mjumuisho ya skuli/mipango ya skuli za majaribio inaweza kuwasilishwa kwa kutumia PawaPointi au wakufunzi wa Jumuiya za Watu wenye Ulemavu wanaweza kuelezea kinachoendelea katika wilaya zao/maeneo yao. Katika hatua ya kupanua utekelezaji wawakilishi wa Kamati za Elimu Mjumuisho za Skuli,

mratibu wa elimu mjumuisho na/au walimu wakuu wa skuli za majaribio wanaweza kuelezea mbinu wanazotumia. Ni muhimu sana kujielekeza zaidi katika mbinu za kusaidia uhamaji katika nyakati za migogoro na ukame, na pia safari ya kurudi skuli kufuatia skuli kufunguliwa baada ya janga la Uviko.

### Katika somo hili washiriki:

ü Wataangalia mbinu tofauti za kusaidia uhamaji jumuishi.
ü Kujadili fursa za ushirikiano na skuli za majaribio/au Kamati za Ujumuishaji za Skuli kuwatambua wanafunzi walio nje ya skuli na kusaidia uhamaji jumuishi.

## Zoezi la 6.1: Kutumia sera kusaidia uhamaji jumuishi.

1 dakika 60

### Maelekezo

- Wakumbushe washiriki kuwa katika Somo la 2 tuliangalia baadhi ya sera muhimu ambazo zinalinda haki za watoto walio nje ya skuli kupata elimu Zanzibar.
- Waambie kuwa hivi sasa tutaangalia jinsi gani tunaweza kutumia sera hizi kusaidia na kushawishi elimu jumuishi.
- Waombe washiriki wajigawe katika makundi mawili.
- Waambie washiriki kuwa wataigiza mkutano baina ya Kamati ya Maendeleo ya Shehia/ Kamati ya Shehia (SC) ambayo Jumuiya ya Watu wenye Ulemavu (iliyoteuliwa na Jumuiya nyengine kwa ajili ya jambo hili) imeomba kushiriki, na watendaji wa serikali wanaohusika na elimu ya makuzi ya awali.
- Wape washiriki wa kila kikundi nakla ya **Kielelezo nam. 6.1: Kutumia sera kushawishi mabadiliko.** Soma maelezo ya igizo yaloyomo katika kitini ili kila mtu afahamu yanahusu nini na nini wanahitajika kufanya.
- **Hakikisha kwamba vikundi vyote vina:**
  - o Nakala ya **Katiba ya Zanzibar (Kielelezo nam. 2.2a).**
  - o Kifungu cha 24 cha **Mkataba wa Umoja wa Mataifa wa Haki za Watu wenye Ulemavu (Kielelezo nam. 2.2b).**

**Pawapointi** — **Somo la 6: slaidi ya 1: maelekezo ya igizo**

- Waambie washiriki kwamba watumie kiasi cha dakika 10 wakijiandaa kwa ajili ya igizo na kufikiria watakavyojigawa katika nafasi mbalimbali. Fuatilia hilo na wasaidie ikihitajika.
- Waambie washiriki waanze igizo lao. Watakuwa na dakika 35 kwa ajili ya igizo.
- Wakati wa igizo fuatilia na sikiliza mambo ya msingi na hoja zitakazojengwa. Unaweza kuhitaji kuzinukuu wakati wa mjadala.

**Pawapointi** — **Somo la 6 slaidi ya 2: Maswali ya mjadala baada ya igizo**

- Baada ya vikundi kukamilisha maigizo, waombe washiriki wakae pamoja tena. Onesha maswali yaliyopo kwenye slaidi na waombe washiriki wote kujadili maswali hayo:
    - ü Sera hizi mbili zilisaidia vipi mjadala unaohusu watoto walioathirika na majanga uliofanyika baina ya kamati ya maendeleo ya shehia/ kamati ya shehia, jumuiya ya watu wenye ulemavu na watendaji wa masuala ya elimu kutoka serikalini?
        - § Kama sera hizo zilisaidia, zilisaidia vipi?
        - § Iwapo hazikusaidia, kwa nini unasema hivyo?
    - ü Je! Hii inaweza kutokea katika maisha halisi?
    - ü Kuna suluhisho lolote la maana lililopatikana kupitia mjadala ambalo litasaidia kuwarudisha watoto skuli na kuwasaidia wale ambao tayari wapo skuli?
    - ü Kuna fikra zozote nyengine zilizoibuka kutokana na igizo ambazo zinaweza kuzisaidia Jumuiya za Watu wenye Ulemavu katika suala la uhamaji jumuishi? Ijapokuwa igizo linahusu elimu ya makuzi ya awali, vikundi vinaweza kufikiria sera au maelezo ya dhamira ya sera ambayo wangependa kuyaona kuhusu watoto walio nje ya skuli kwa jumla?

## Zoezi la 6.2a: Simulizi ya Musa na Yasmiin

1 dakika 30

### Maelekezo

- Waambie washiriki kuwa utazisoma simulizi mbili kwa sauti. Simulizi zinawahusu wanafunzi ambao wanapitia changamoto ya kuhamia skuli au kuhama skuli moja kwenda nyengine.
- Isome simulizi ya Musa kwanza. **Kielelezo nam. 6.2a: Simulizi ya Musa.** Isome taratibu na kwa ufasaha ili kila mmoja aweze kuifahamu.
- Onesha slaidi ya PawaPointi yenye maswali kwa ajili ya mjadala (chini) na waulize washiriki maswali kwa wote, ukiandika majibu yao katika flipchati. Ukihisi washiriki wanahitaji muda wa kutafakari, waombe wajadili maswali hayo katika jozi kwanza.

**Pawapointi** **Somo la 6: slaidi ya 3**

- Musa ana mahitaji yepi?
- Mbinu zipi zinaweza kusaidia kukidhi mahitaji haya?
- Je! Skuli/kamati ya ujumuishi ya skuli inaweza kufanya nini?
- Je! Jumuiya ya Watu wenye Ulemavu inaweza kusaidiaje kufanikisha uhamaji?

- Baadae soma simulizi ya Yasmiin, **Kielelezo nam. 6.2: Simulizi ya Yasmiin,** na fuata hatua zilezile. Kwa mara nyengine, ukiandika majibu ya washiriki katika flipchati.
- Mwisho waulize washiriki iwapo wanawajuwa watoto wanaopitia changamoto kama hizi katika mazingira yao?

**Tanbihi kwa mkufunzi:**

Lengo la zoezi hili ni kupokea mawazo kuhusu mbinu tofauti ili kusaidia uhamaji jumuishi. Hakuna majibu sahihi au yasio sahihi kwa kuwa kuna mbinu tofauti zinazoweza kutumika kutatua tatizo hilo hilo. Ukiandika mawazo yao kwenye flipchati kutasaidia kujiandaa kwa zoezi la 6.3.

## Zoezi la 6.3: Mikakati ya uhamaji jumuishi

1 dakika 60

- Wakumbushe washiriki kuwa uhamaji jumuishi wenye mafanikio unahitaji **usaidizi kutoka nyumbani mpaka skuli.** Unahitaji ushirikiano baina ya skuli na wazazi na familia ili kurahisisha uhamaji, hasa kwa wanafunzi wenye mahitaji ya ziada.
- Gawa kadi kutoka kwenye **Kielelezo nam. 6.3a: kadi za changamoto** na **Kielelezo nam. 6.3b: kadi za mikakati** kwa kila kikundi. Kadi kutoka **Kielelezo nam. 6.3a** na **Kielelezo nam. 6.3b** ziwe za rangi tofauti.
- Waambie washiriki kwamba wanaweza kuzitambua baadhi ya 'changamoto' kwa kuwa baadhi yake ni zile ambazo waliziona hapo kabla katika Somo la 5 zikielezea hali tofauti za uhamaji walizopitia wanafunzi.

**Pawapointi** **Somo la 6: slaidi ya 4: Mikakati ya uhamaji jumuishi**

- Waombe washiriki waoanishe mikakati na changamoto ambazo zinaweza kutatua. Wakumbushe kuwa hakuna mbinu moja kwa kila kadi ya changamoto; mikakati kadhaa inatatua changamoto kadhaa, kwa hivyo washiriki waziweke katika mafungu kuonesha ile mikakati ambayo inaoana na changamoto mbalimbali.
- Waambie washiriki kwamba mikakati hiyo ni pamoja na ile ambayo inaingia katika majukumu ya kamati ya Elimu Mjumuisho ya skuli ikishirikiana na Jumuiya za Watu wenye Ulemavu na/au jumuiya nyengine.
- Katika kadi zisizokuwa na maandishi, washiriki wanaweza kuandika changamoto za ziada na mikakati, iwapo watagundua kitu kipya mpya wakati wa mjadala.
- Baada ya dakika 15-20 waombe washiriki watowe mrejesho mbele ya washiriki wote kuhusu maamuzi waliofanya kuhusu mikakati sahihi na kisha wajadili:
  - ü Je! Ni mikakati ipi yenye ufanisi?
  - ü Katika ngazi ya mwanafunzi/skuli/jamii, ni jukumu/wajibu wa nani kutekeleza kila aina fulani ya mkakati?
  - ü Mikakati ipi ambayo inaweza kutumiwa na Jumuiya za Watu wenye Ulemavu?



Uoanishaji wa mikakati na changamoto katika warsha iliyafanyika Zanzibar

[Maelezo ya picha: Washiriki wanawake na wanaume wakiwa katika vikundi. Katika kila kikundi kuna kadi za mikakati na changamoto ambazo washiriki wanazitazama na kuzijadili. Vilevile mkufunzi amesimama pembezoni mwa moja kati ya meza za washiriki akisikiliza mjadala]

Kwa kumbukumbu za mkufunzi, jeduwali lililopo hapa chini limependekeza aina ya changamoto na mikakati zinazoweza kuoanishwa pamoja:

| Changamoto | Mikakati |
|---|---|
| Siijui au sijaona njia rahisi ya kufika kwenye skuli yangu mpya. | Fuatana na mwanafunzi ambae ndio kwanza anajiunga na skuli, mpe ramani na mtafutie wenzake (kwa mfano, 'marafiki wa darasani') wa kumsaidia kujua njia. |
| Skuli niliyoandikishwa ipo mbali na nyumbani na nina hofu ya kwenda peke yangu. | Hamasisha tabia ya kushirikiana ambapo watoto wanatembea pamoja kwenda na kurudi skuli. |
| Wazazi wangu ni masikini, hawamudu kunilipia skuli. | Wahamasishe wazazi kuwaandikisha watoto wao katika skuli za serikali ambako gharama ni ndogo. |

<table>
<tr><th>Changamoto</th><th>Mikakati</th></tr>
<tr><td>Wazazi wangu hawaoni umuhimu wa mimi kuendelea na elimu ya sekondari. Wanataka nifanye kazi.</td><td rowspan="2">Endelea kujenga uelewa kwa familia na jamii kuhusu haki ya watoto wote kupata elimu na waelimishe wazazi kuhusu faida ya muda mrefu ya watoto kupata elimu.</td></tr>
<tr><td>Nilianza biashara ya kuuza mikate wakati wa Korona na sioni haja ya mimi kurudia skuli</td></tr>
<tr><td rowspan="2">Niliolewa kipindi cha karantini ya Uviko na najisikia aibu kurudi skuli kwa kuwa wenzangu watanicheka.</td><td>Hakikisha wanafunzi wanaoishi katika mazingira magumu (kwa mfano, watoto wa kike waliozaa utotoni) wanapata huduma za unasihi.</td></tr>
<tr><td>Rejea na utumie sera ya serikali na muongozo kusaidia uhamaji jumuishi. (kwa mfano, serikali imeweka miongozo kwa watoto wa kike na wa kiume waliozaa utotoni kurudi skuli).</td></tr>
<tr><td>Wazazi wangu hawajui kuwa natakiwa kufanya kazi za nyumbani ninaporudi kutoka skuli. Wanatarajia nimlee ndugu yangu na kufanya kazi za nyumbani.</td><td>Waalike wazazi wote/walezi katika siku ya kutembelea skuli/kikao cha udahili ambapo taarifa hutolewa kabla ya mtoto hajapangiwa darasa. Elezea matumaini ya skuli na jinsi gani wazazi na walezi wanaweza kushirikikshwa katika kusaidia elimu ya watoto wao.</td></tr>
<tr><td>Kama mtoto wa kike, tayari nimekuwa, nalazimika kufanya kazi za nyumbani zaidi. Hii hunifanya nichelewe kufika skuli na kuadhibiwa.</td><td>Waombe walimu na/au mratibu wa elimu mjumuisho kuwatembelea baadhi ya wanafunzi ili kujua mahitaji yao na hali za familia zao.</td></tr>
<tr><td>Sijazoea kuwa mbali na wazazi wangu siku nzima.</td><td>Skuli zinaweza kuwakaribisha wazazi/walezi (hasa katika skuli za maandalizi na madarasa ya mapokezi) ili kuwatuliza watoto wao. Wahusishe wazazi/walezi katika kutengeneza ratiba ya uhamaji na mambo ya kufanya.</td></tr>
</table>

| Changamoto | Mikakati |
|---|---|
| Wazazi wangu hawaufahamu ulemavu wangu na wana hofu kwamba sitopata msaada ninaouhitaji katika mazingira ya skuli. | Kamati ya skuli ya elimu mjumuisho iwahusishe wajumbe wa jumuiya za watu wenye ulemavu ili kusaidia kuongeza ufahamu kuhusu ulemavu katika jamii na kusaidia uhamaji wa wanafunzi wenye ulemavu skuli. |
| Nataka kujiunga na chuo cha mafunzo ya amali. Sijui chuo kipi ni jumuishi kwa watu wenye ulemavu. Pia katika skuli yangu hakuna anayejua. | Hakikisha skuli za sekondari zina taarifa kuhusu vyuo vya elimu ya juu ambavyo vinafikika na vinazingatia ujumuishi. |
| | Hakikisha skuli za sekondari, taasisi za elimu ya juu na vyuo vya mafunzo ya amali vinatoa muongozo wa kada za kusomea, vitowe ushauri sahihi na wa kuhamasisha kwa wanafunzi wenye mahitaji ya ziada. |
| Sikuwahi kuiona skuli yangu mpya mpaka siku niliojiunga. Nilikuwa na hofu. | Wasaidie wanafunzi kutembelea darasa lao jipya/skuli na wajuwe mazingira yake, wawajuwe watu na taratibu kabla hawajajiunga rasmi. |
| | Skuli zinaweza kuandaa 'siku ya utambulisho' katika muhula wa mwisho kabla ya siku rasmi ya wanafunzi kufika skuli. Katika siku hizi wanafunzi wapya watakutana na walimu watakaowasomesha mwaka ujao, kushuhudia baadhi ya masomo yakiendelea, na kukutana na wanafunzi wenzao watarajiwa kutoka katika skuli nyengine. |
| | Andaa shughuli za kujenga urafiki katika siku za awali za masomo. |
| Sijisikii kuwa ni sehemu ya skuli hii. | Hakikisha wanafunzi wapya wote wanashirikishwa katika mambo ya ubunifu na burudani yaliomo katika mtaala na nje ya skuli ili waweze kuzoeana na jamii. |

| Changamoto | Mikakati |
|---|---|
| Nafanyiwa fujo na huwa naogopa hasa wakati wa mapumziko na chakula cha mchana. | Andaeni sera ya kukomesha vitendo vya kuashiria uchokozi na hakikisha watu waliopewa jukumu la kusimamia nyakati za mapumziko na chakula cha mchana wanapewa taarifa kuhusu wanafunzi wapya. |
| | Hakikisha kila mmoja anajuwa aende wapi (hasa wakati wa nyakati za mapumziko) iwapo hawajisikii salama. |

## Zoezi la 6.4: Fursa za ushirikiano: Jukumu gani linaweza kutekelezwa na Jumuiya za Watu wenye Ulemavu kuzisaidia skuli?

1 dakika 90

Zoezi hili lina zihusisha skuli za majaribio kuelezea mbinu walizobuni kuwatambua wanafunzi walio nje ya skuli na kusaidia uhamaji jumuishi kwa ujumla.

Katika ngazi ya taifa muhutasari wa shughuli zinazofanywa na kamati ya elimu mjumuisho ya skuli/mipango ya skuli ya majaribio inaweza kuelezwa kwa kutumia PawaPointi au wakufunzi wa Jumuiya za Watu wenye Ulemavu wanaweza kuelezea kinachoendelea katika wilaya zao. Katika ngazi ya kupanua utekelezaji wawakilishi wa Kamati moja ya Ujumuishi ya Skuli, Mratibu wa Elimu Mjumuisho na/au walimu wakuu wa skuli za majaribio wanaweza kuelezea mbinu walizobuni.

Itakuwa jambo la maana hasa kulenga katika mikakati ya kusaidia uhamaji uliosababishwa na kuhama au kulazimika kuhama kufuatia mgogoro au ukame au hali ya mabadiliko ndani ya familia (ugonjwa au kifo kinachopelekea malezi ya watoto kuhamishwa kutoka kwa wazazi na kukabidhiwa mtu mwengine katika familia kama vile ndugu au wajomba na shangazi kwa mfano), na pia uhamaji baina ya ngazi au madarasa tofauti.

**Pawapointi** **Somo la 6: slaidi ya 5: Maelezo kutoka katika skuli za majaribio**

- Muite muwakilishi wa Kamati ya Elimu Mjumuisho ya Skuli au mwalimu mkuu kuelezea kile wanachokifanya ili kuwatambua watoto walio nje ya skuli na kusaidia uhamaji jumuishi katika skuli yao. Waombe walenge zaidi kwenye mbinu ambazo zinahitaji ushirikiano na wadau wa skuli/jumuiya nyengine. Wasilisho lao lilenge katika maeneo yafuatayo:
  - **Je! Kamati ya Elimu mjumuisho imefanya nini kuwatambua wanafunzi walio nje ya skuli?**
  - **Wana mikakati gani ya kusaidia uhamaji jumuishi?**
  - **Kuna mikakati yoyote iliyobuniwa baada ya skuli kufunguliwa baada ya kufungwa kutokana na sababu mbalimbali (m.f. mafuriko, ukarabati wa miundombinu n.k.), ili kuwasaidia wanafunzi kurejea skuli?**
  - **Kwa nama gani Jumuiya za Watu wenye Ulemavu zinaweza kusaidia?**
- Karibisha maswali na mjadala kutoka kwa washiriki baada ya mawasilisho.
- Sisitiza juu ya umuhimu wa usaidizi ulioratibiwa, ambapo skuli zinafanya kazi sambamba na taasisi nyengine, wadau na taasisi za huduma kuhakikisha ufikiaji wa elimu kwa wanafunzi na familia zinazohama.
- Baadae, wakaribishe washiriki kutembelea vikundi vya wilaya/shehia zao. Mtakapopanua utekelezaji fikirieni kuhusu namna bora ya kutengeneza makundi au mnaweza kuamua kujadiliana wote kama kundi moja.

**Pawapointi** **Somo la 6: slaidi ya 7: Majukumu gani yanayoweza kutekelezwa na Jumuiya za Watu wenye Ulemavu?**

- Waambie washiriki kuwa kwa dakika 30-40 zijazo watajadili katika vikundi vyao wakilenga swali:

  **Jukumu lipi ambalo Jumuiya za Watu wenye Ulemavu zinaweza kulitekeleza katika kuwatanbua watoto walio nje ya skuli na kusaidia uhamaji jumuishi?**
- Karibisha ushauri mchache kutoka kwa washiriki wote na uandike kwenye karatasi ya flipchati.
- Baadae onesha slaidi yenye **majukumu muhimu ambayo Jumuiya za Watu wenye Ulemavu zinaweza kutekeleza** katika kuzisaidia skuli kuwatambua wanafunzi walio nje ya skuli na kusaidia uhamaji jumuishi:

- **Kutafuta na kukusanya taarifa ili kuleta ushahidi kwa ajili ya kuleta mabadiliko (kwa kutumia uzowefu ulioyokana na zoezi la awali la ukusanyaji wa taarifa na data baada ya moduli ya mwanzo).**
- **Kurahisisha ushirikiano  ili kujenga umoja madhubuti na mtandao kwa ajili ya mabadiliko kwa mfano kukusanya rasilimali za jamii.**
- **uelewa kuhusu mabadiliko gani yanayohiyajika kwa ajili ya elimu jumuishi.**
- **Kutumia sera kushawishi ufanyaji maamuzi kwa ajili ya mabadiliko**
- **Kufuatilia na kusaidia michakato ya mabadiliko kwa ajili ya elimu mjumuisho.**

- Waombe washiriki katika vikundi vyao kujadili swali la msingi na majukumu haya tofauti kwa kina. Waombe washiriki:
  - Kufikiria kilichowasilishwa na skuli/Kamati za Mjumuisho za Skuli.
  - fikiria changamoto mbalimbali na mbinu zilizojadiliwa katika siku mbili zilizopita.
- Washiriki katika vikundi vyao waandike mawazo yao kwenye flipchati, huku wakitoa mifano ikiwezekana.
- Baada ya dakika 30, katika majadiliano, viombe vikundi kuelezea mawazo yao na karibisha michango na maswali kutoka kwa washiriki wote kwa ujumla.

# Vielelezo na vitini

Moduli ya

# 3

# Kielelezo nam. 1.1: Ufafanuzi wa vipengele: Ni nani wanafunzi walio nje ya skuli na kwa nini wapo nje?

## 1. Aina mbalimbali ya vikwazo vinavyozuia wanafunzi kwenda skuli

Kuna aina mbalimbali mtambuka ya vikwazo vinavyozuia wanafunzi kwenda skuli. Vikwazo hivyo vimegawanywa katika makundi matatu.

a) **vikwazo vya kimazingira na nyenzo;**

b) **vikwazo vya kimtazamo na Imani;**

c) **Vikwazo vya kisera na kiutendaji.**

Inawezekana kwamba umewahi kusoma kuhusu vikwazo vya ujumuishi katika mafunzo mengine kuhusu elimu mjumuisho. Vikwazo vya ujumuishi ni vikwazo vinavyoathiri **uwepo** wa wanafunzi skuli, **ushiriki** wao katika mchakato wa kujifunza, na **mafanikio** yao.

Kwa kukukumbusha tu, vikwazo hivyo ni:

- **Vikwazo vya kimazingira:** kwa mfano, majengo ya skuli, mazingira ya skuli na vyoo ambavyo havifikiki;
- **Vikwazo vya rasilimali:** kwa mfano, uhaba wa walimu, idadi kubwa ya wanafunzi darasani;
- **Vikwazo vya kimtazamo:** kwa mfano, hofu, fedheha, aibu, kuonekana huna bahati, matarajio madogo;
- **Vikwazo vya kisera:** kwa mfano, ratiba za skuli zisizo nymbulifu; utumiaji wa lugha ngeni;
- **Vikwazo vya kiutendaji:** kwa mfano, ukosefu wa mbinu shirikishi na husishi za kufundishia.

Katika moduli hii ya mafunzo tutaangalia kwa ukaribu vikwazo vinavyosababisha wanafunzi kuwa nje ya skuli – ijapokuwa vingi vyao vinalingana na vikwazo vya ujumuishaji.

## a) **Mazingira na nyenzo**

Neno mazingira linamaanisha miundombinu iliyojengwa na maumbo ya asili. Hii inaweza kuhusisha eneo maalumu, nchi, mji, au kijiji; mjini au kijijini.

Pahali ambapo mwanafunzi anaishi panaweza kuathiri mahudhurio yake ya skuli. Kwa mfano, kiujumla kuna skuli nyingi zaidi na zinazofikika kwa urahisi katika maeneo ya mijini kuliko vijijini. Kwa hivyo, kuna wanafunzi wengi zaidi walio nje ya skuli katika maeneo ya vijijini kuliko mijini.[4] Katika maeneo ya vijiji vilivyoko mbali ambapo masafa baina ya jamii ni makubwa na usafiri una shida (kwa mfano, milima mirefu ambayo ni vigumu kuipanda), ukosefu wa miundombinu (kwa mfano, Barabara na madaraja) na mabadiliko ya tabia nchi (kwa mfano, mafuriko ya mara kwa mara), inaweza kusababisha kuwa vigumu kwa baadhi ya wanafunzi kuzifikia skuli chache zilizokuwepo. Vikwazo hivyo vya kimazingira huchangia wanafunzi wawe nje ya skuli katika maeneo hayo.

**Rasilimali –** hujumuisha rasilimali za **kiuchumi/vifaa, watu**, na **kiutamaduni –** zinaweza kuathiri mahudhurio ya wanafunzi skuli. **Rasilimali za kiuchumi** za familia na jamii huamua iwapo familia itamudu kumpeleka watoto wao skuli au iwapo jamii itakuwa na skuli ambayo watoto wa jamii hiyo wataweza kuhudhuria. Familia masikini zinaweza kuwa zinategemea watoto wao wafanye kazi ili ziweze kuishi na hivyo kutoa kipaumbele kwa kazi badala ya elimu. Skuli zilizopo katika maeneo masikini inawezekana zikawa na uhaba wa vifaa vya kufundishia na kujifunzia, madarasa na nyenzo nyengine, ili kukidhi mahitaji ya wanafunzi wote walio katika umri wa kwenda skuli katika eneo hilo.

Uhaba wa walimu, au walimu waliopatiwa mafunzo ni **kikwazo cha rasilimali watu** ambacho huathiri ufikiaji wa elimu kwa wanafunzi.

Familia zisizokuwa na **rasilimali za kitamaduni,** kama vile kusoma na kuhesabu, ambao umetokana na kupata elimu rasmi, inaweza kuzuia vigumu kuwasaidia watoto wao kujifunza na hii inaweza kupelekea wanafunzi wasihudhurie skuli, au kuacha kabla ya kumaliza (hii pia inaungana na mitazamo na uzoefu).

## b) Mitazamo na imani

Mitazamo ya watu, familia, wanakijiji na jamii inaweza kuwa ni sababu kubwa ya kuwafanya wanafunzi wawe nje ya skuli. Kwa mfano, baadhi ya familia na jamii zinaamini wanafunzi wenye ulemavu hawapaswi kwenda skuli. Katika jamii nyengine, familia zina mtazamo wa kwamba watoto wa kike wanapaswa kubaki nyumbani na sio kwenda skuli. Wakati mwengine wanafunzi

wanachokozwa na wenzao (au walimu) kwa sababu wanatoka katika jamii fulani, wafuasi wa dini fulani au wanazungumza lahaja fulani. Wanafunzi wanaochokozwa wanaweza kuacha skuli kuepuka kudhalilishwa.

Wazazi na walezi ambao wao wenyewe hawajawahi kwenda skuli inawezekana wasione umuhimu wowote wa kuwapeleka watoto wao skuli. Tafiti zinaonesha kwamba uzoefu wa mama kuhusiana na elimu ni sababu muhimu inayoamua iwapo mwanafunzi aandikishwe skuli au la[3]. Utafiti wa UNESCO (2005) umeonesha kwamba, duniani kote, watoto waliofikia umri wa kuandikishwa skuli ambao mama zao hawakuwahi kusoma skuli uwezekano wa kutoandikishwa skuli ni mara mbili zaidi ya watoto ambao mama zao walisoma skuli. Mara nyingi ni ukosefu wa elimu au uelewa na hofu unaopelekea mitazamo hasi.

### c) Sera na utekelezaji

Sera za nchi, jamii, na skuli zinaweza kuchangia tatizo la watoto wan je ya skuli. Kwa mfano, ikiwa nchi haina sera ya elimu bure, wanafunzi wengi wanaweza kukosa elimu kwa sababu wao, wazee wao na walezi hawamudu kulipia ada za skuli. Iwapo sera ya skuli inalazimisha ratiba ya masomo ianze mapema na haipo nyumbulifu kwa wanafunzi wanaochelewa kufika skuli, sera hii inaweza kusababisha kuachwa wanafunzi wanaochelewa kwa sababu wanalazimika kutembea masafa marefu kwenda skuli.


Utekelezaji wa elimu, hasa mchakato wa kufundisha na kujifunza, huathiri hali ya mwanafunzi ya kujifunza. Baadhi ya wanafunzi huamua wasiende skuli kwa sababu wanahisi kukosa uchangamfu, haiwavutii au hawafurahii. Wanaweza kuhisi kwamba elimu haikidhi mahitaji yao au ina umuhimu mdogo au maana katika maisha yao. Mbinu za ufundishaji zinazotoa nafasi kwa mwalimu zaidi, na kukariri kunaweza kusababisha wanafunzi wapoteze shauku ya kujifunza na kuamua kuacha skuli. Wanafunzi pia wanaweza kuacha skuli kwa kuogopa adhabu. Mambo haya yote yanahusiana na utekelezaji, na mara nyingi mbinu mbaya za kufundishia zinatokana na mafunzo duni ya walimu.

## 2. Vikwazo maalumu vinavyozuia wanafunzi kwenda skuli

Kuna vikwazo maalumu vinavyozuia wanafunzi kujifunza. Vikwazo vyote vya jumla na maalumu ambavyo huathiri mahudhurio ya wanafunzi skuli vinahusiana, na hili huwa bayana pale tunapoangalia sababu zake.

---

[3] UNESCO



Upungufu wa walimu waliopata mafunzo vizuri



Walimu wachache wenye mafunzo duni na darasa kubwa



Walimu wachache wenye mafunzo duni na darasa kubwa




Wanafunzi wanatoroka skuli na kufanya kazi ya kusafisha na kuuza samaki



Wazazi au walezi hawaoni umuhimu wa kupeleka watoto wao skuli.




Skuli ipo mbali na makaazi ya wanafunzi

Badala ya kuwepo sababu moja ya kawaida inayosababisha mwanafunzi awe nje ya skuli, kiuhalisia kuna mlolongo mrefu wa sababu na athari. Kwa mfano, uhaba wa walimu wenye taaluma sahihi unaweza kupelekea skuli kuwa na mwalimu mmoja mwenye elimu duni anaeshughulikia madarasa yenye idadi kubwa ya wanafunzi. Hii hupelekea wanafunzi kupata elimu isiyo na ubora; ambayo itapelekea baadhi ya wanafunzi kuacha masomo kwa sababu hawanufaiki, na/au wazazi/walezi wao kuhisi haina maana kuwaandikisha skuli. Pia skuli inaweza kuwa masafa marefu kutoka wanakoishi baadhi ya wanafunzi jambo ambalo huathiri mahudhurio yao.

Katika mfano wa hapo juu, tunaweza kusema kwamba ufundishaji duni ni sababu ya wanafunzi kuacha skuli. Hata hivyo, hii haiondoi sababu nyengine mbali na ufundishaji duni usiozingatia weledi (kama vile ukosefu wa walimu, kukosa ujuzi wa mbinu ya kulisimamia darasa lenye idadi kubwa ya wanafunzi, na mbinu za kufundishia zinazomlenga mwanafunzi), au sababu nyengine zinazochangia (kama vile mitazamo ya wazazi/walezi na uzoefu wa elimu rasmi).

Baadhi ya vikwazo maalumu zaidi vinavyozuia wanafunzi kwenda skuli ni:

- umri;
- migogoro na majanga;
- ulemavu;
- ukabila, dini na utamaduni;
- jinsia;
- afya;
- lugha;
- uhamaji;
- umasikini.

## Umri

Umri unaweza kupelekea mwanafunzi kuacha skuli. Wanafunzi wanapochelewa kuanza skuli (wakaanza baadae kuliko wenzao), au kurudia madarasa, kuna uwezekano mkubwa wa kuacha skuli kabla ya kumaliza[6]. Katika muktadha mwengine kuna shinikizo kwa wanafunzi kufanya kazi katika umri mdogo, na hivyo kutohudhuria skuli.

## Migogoro na majanga

Migogoro (kama vile vita vya wenyewe kwa wenyewe) na majanga (kama vile mafuriko na matetemeko ya ardhi) yanaweza kuwa sababu kubwa ya kuwafanya wanafunzi wawe nje ya skuli. Skuli inaweza kuwa imepata athari, imeharibiwa kabisa, au haipo. Kutembea kwenda na kurudi skuli inawezekana ikawa si salama au haiwezekani kabisa. Hata pale ambapo skuli zipo wazi, inawezekana zisiwe sehemu salama kwa wanafunzi. Katika baadhi yan chi wanafunzi wanalazimishwa kupigana vita kama wanajeshi watoto.

## Ulemavu

Wanafunzi wenye ulemavu mara nyingi huwa wanatengwa. Hii inawezekana kwa sababu ya:

- Mitazamo na imani – katika baadhi ya maeneo watu wanaamini kwamba wanafunzi wenye ulemavu hawawezi, au hawapaswi, kupelekwa skuli.
- Ufikiaji – skuli inawezekana ziwe hazifikiki kwa baadhi ya wanafunzi wenye ulemavu
- Ukosefu wa nyenzo na uwezo – baadhi ya skuli hukosa (au huamini kuwa hawana) vifaa na uwezo, idadi ya wafanyakazi na mafunzo waliopatiwa, ili waweze kuwajumuisha ipasavyo wanafunzi wenye ulemavu.

## Kabila, dini na utamaduni

Wanafunzi wanaweza kufukuzwa skuli kwa sababu ya kabila au dini. Jambo hili mara nyingi huwaathiri watu wanaotoka katika makabila madogo au madhehebu yasio maarufu ya kidini. Mgogoro wa kikabila au kidini unaweza kusababisha hali ikawa mbaya zaidi. Baadhi ya wanafunzi wanaweza kuacha skuli kwa kubaguliwa na kufanyiwa fujo kutokana na kabila au dini zao. Baadhi ya wazazi/walezi wanaweza kuamua kutowaandikisha watoto wao skuli kwa sababu mafundisho yake hayaendani na imani zao za kidini.

## Jinsia

Ijapokuwa hali inaimarika, bado kuna watoto wengi zaidi wa kike kuliko wa kiume ambao hawaendi skuli duniani kote. Baadhi ya maeneo yana idadi kubwa ya watoto wa kike walio nje ya skuli, na maeneo mengine yakiwa na uwiano sawa wa watoto wa kike na wa kiume walio nje ya skuli, au hata asilimia kubwa ya watoto wa kiume, hasa katika nchi zenye maendeleo makubwa ya viwanda.[4]

[4] UNESCO, 2005

Mitazamo potofu na mila zinazofanana na mitazamo hiyo zinaendelea kuathiri watoto wa kike zaidi na uwezekano wa kupata huduma za elimu. Kwa mfano, ndoa za utotoni, ambapo watoto wa kike wenye umri wa miaka nane au tisa katika baadhi ya nchi wanalazimishwa kuolewa, kwa kiasi kikubwa zinapunguza uwezekano wa wao kuhudhuria au kudumu skuli.

## Afya

Afya duni, inayosababishwa na lishe duni na maradhi, husababisha wanafunzi wengi kuwa nje ya skuli. Kuna unyanyapaa ambao huambatana na maradhi fulani, kwa mfano VVU na UKIMWI, ambao huchangia wanafunzi kufukuzwa skuli. Afya, mara nyingi ni matokeo ya moja kwa moja ya vikwazo vyengine, kama vile umasikini, majanga na migogoro.

## Lugha

Lugha ya kufundishia skuli inaweza kuwa kikwazo iwapo itakuwa ni tofauti na lugha inayozungumzwa nyumbani kwa mtoto ('lugha ya asili'). Wanafunzi hawa wanaweza kupata shida ya kujifunza na kuamua kuacha skuli. Hii mara nyingi huwaathiri wanafunzi kutoka katika makabila madogo. Masuala ya lugha mara nyingi hunasibishwa na ukabila, dini na utamaduni.

## Kuhama

Kuhama kwa watu kutoka eneo moja kwenda jengine, iwe kwa sababu za kiuchumi, kukimbia majanga na migogoro au kwa sababu za kiutamaduni, kuna athari kubwa katika elimu ya mwanafunzi. Wanafunzi wanaolazimika kuhama kwa sababu ya majanga na migogoro katika nchi zao mara nyingi huishia katika kambi za wakimbizi katika nchi nyengine ambako uwezekano wa kupata elimu unaweza kuwa finyu. Wanafunzi ambao huwa ni wakimbizi wa ndani katika nchi yao wenyewe, mara nyingi huwa na fursa ndogo zaidi, kama ikiwepo, ya kupata elimu rasmi.


Hata wanafunzi wanaohama kwa sababu za kiuchumi wanaweza kujikuta wapo nje ya skuli. Wanaweza kukabiliwa na vikwazo vya lugha au utamaduni, wazazi/walezi wao inawezekana wasimudu gharama za kuwasomesha.

## Umasikini


Katika nchi nyingi duniani umasikini ndio kikwazo kikuu ambacho huwaacha wanafunzi nje ya skuli. Katika maeneo masikini mara nyingi huwa na skuli chache na nyenzo chache za kufundishia na walimu wachache wenye taaluma

duni. Changamoto hizi husaidia watoto wawe nje ya skuli. Baadhi ya familia hazimudu kuwaandikisha watoto wao skuli na badala yake wanafunzi waweza kulazimika kufanya kazi. Duniani kote, ijapokuwa sera husema kwamba elimu ni bure, mara nyingi huwepo gharama zilizojificha, kama vile sare na vitabu.

# Kielelezo nam. 1.2: Vikwazo vinavyohusina



Upungufu wa walimu waliopata mafunzo vizuri



Walimu wachache wenye mafunzo duni na darasa kubwa



Walimu wachache wenye mafunzo duni na darasa kubwa




Wanafunzi wanatoroka skuli na kufanya kazi ya kusafisha na kuuza samaki



Wazazi au walezi hawaoni umuhimu wa kupeleka watoto wao skuli.




Skuli ipo mbali na makaazi ya wanafunzi

# Kielelezo nam 1.3a: Orodha ya vikwazo vinavyowazuia wanafunzi kujifunza

## Aina za vikwazo vinavyowazuia wanafunzi kwenda skuli

- Mazingira na Rasilimali
- Mitazamo na Imani
- Sera na Utekelezaji

## Aina maalumu ya vikwazo vinavyowazuia wanafunzi kwenda skuli

- Mitazamo kuhusu umri
- Mitazamo kuhusu skuli
- Migogoro na majanga
- Mitazamo kuhusu ulemavu
- Mitazamo kuhusu ukabila, dini na utamaduni
- Mitazamo kuhusu jinsia
- Afya
- Lugha
- Uhamaji
- Umasikini


## Kielelezo nam. 1.3b: Picha ya vikwazo vinavyowazuia wanafunzi kujifunza





[Maelezo ya picha:  majengo ya skuli matatu yaliogeuzwa kuwa kambi ya wanajamii walioathirika na mafuriko, kuna wanawake watatu, wawili wamekaa na mmoja amesimama pembeni na wanaume wawili waliokaa mmoja akiwa amevaa kanzu nyeupe wanaonekana wanajadili mambo muhimu. Katika vyumba vya madarasa kunaonesha watu wamo ndani, wengine wanaingia katika vyumba hivyo. Mbele ya majengo hayo kuna bango lililoandikwa skuli. Pembeni kwa mbali upande wa kushoto kuna majengo yaliobomoka na kuna maji yenye tope tope yaliozunguka maeneo hapo. Pia kuna watoto wawili wanaonekana wanacheza katika tope hizo.]




[Maelezo ya picha: Picha inaonesha njia ndefu ya wapita kwa miguu inayokatisha katikati ya vichaka kwenye ardhi yenye vumbi na mawe. Kuna baadhi ya watoto wa kiume wanachunga mbuzi karibu na njia hiyo. Kwa mbali upande wa kushoto kuna skuli. Kwa mbali upande wa kulia kuna kijiji. Watoto wawili waliovalia sare wanapita katika njia hiyo.]




[Maelezo ya picha: Foleni mbili ndefu, moja ya watoto wa kiume na nyengine ya watoto wa kike wakiwa wamesimama wakisubiri kutumia vyoo. Katika foleni ya watoto wa kiume kuna mtoto mmoja anayetumia gongo la kutembelea na mwengine mwenye ulemavu ualbino. Majengo ya vyoo yanaonekana yamechakaa. Upande wa kushoto, kuna mtoto anaefanya haja ndogo nyuma ya kichaka. Jengo la skuli lipo upande wa nyuma wa eneo hilo.]




[Maelezo ya picha: Darasa lenye idadi kubwa ya wanafunzi huku wanafunzi wengi wakiwa wamekaa kwa kukaribiana sana katika mistari. Mwalimu anaonekana kwa mbali  katika upande wa mbele akiwa anaashiria maandishi yaliopo ubaoni. Kuta za darasa na madarasa yapo katika hali ya uchakavu.]




[Maelezo ya picha: Mwanaume amelala kwenye sofa huku miguu yake ikiwa juu, akizungumza kwenye simu ya mkononi. Ni wazi sio simu ya kazi. Mvulana mdogo aliyevaa mavazi ya shule anashikilia karatasi zenye maandiko akimwelekea mwanaume. Mwanaume anatazama mbali na anainua mkono wake. Uso wake unaonyesha kukasirika.]



[Maelezo ya picha: Mtoto mdogo wa kike anasafisha sakafu kwenye chumba akiwa na ndoo kando yake. Kuna sofa nyuma yake na picha mbili zilizotundikwa ukutani, moja ikionesha watu wanne (watu wazima wawili na watoto wawili) na nyengine inaonesha watoto wawili. Mtoto wa kiume anatembea akipita kando ya mtoto wa kike anaesafisha sakafu. Amevaa sare za skuli na amebeba begi mgongoni. Mtoto wa kike anamuangalia. Anaonekana mwenye huzuni.]





[Maelezo ya picha: Mtoto wa kike aliye katika umri wa kubaleghe, ambae hajavaa sare amembeba mtoto mgongoni. Amesimama nje ya skuli akiangalia ndani. Anaonekana mwenye huzuni. Kuna watoto wawili wa kike waliovaa sare za skuli waliosimama mbele ya skuli wakimuangalia huku wanazungumza.]



[Maelezo ya picha: Mchoro wa ramani ya Afrika. Juu kuna mtu aliyekaa kwenye kiti mwendo huku alama za magurudumu kuashiria mwendo zikiwa nyuma yake. Katikati kuna mwanamke aliyemshika mkono mtoto, nyuma yao kukiwa na alama za nyayo zikiashiria mwendo, na chini kuna mtu anaetembea kuelekea chini, alama za nyayo zikiwa nyuma yake kuashiria mwendo. Watu wote hao ni watu wa kuchora.]




[Maelezo ya picha: Mwanamke mtu mzima amesimama mbele ya wanafunzi waliokaa kwenye madawati akiashiria juu kwa mkono huku akizungumza. Amewaelekezea mgongo wanafunzi. Mbele ya darasa mwanafunzi mmoja anaangalia nje kupitia dirishani na mwanafunzi mwengine amefunika kichwa chake kwa mikono akiwa amelala juu ya dawati.]



[Maelezo ya picha: Mtoto wa kiume amekaa juu ya kiti mwendo peke yake akiangalia chini. Kuna ngazi nyingi nyuma yake zinazoelekea kwenye mlango wa darasa. Kupitia mlangoni mwalimu anaonekana akiendelea kusomesha.]




[Maelezo ya picha: Kuna mwanamme mtu mzima aliyesimama mbele ya darasa akiwa ameshika fimbo ndefu. Anaonekana mwenye ghadhabu. Ameielekeza fimbo kwa yule mtoto wa kiume aliyesimama mbele yake. Mtoto wa kiume ameinamisha kichwa chini. Kuna wanafunzi darasani wanamuangalia. Nje ya darasa lililowazi kuna mtoto wa kiume aliyesimama kwenye uwanja wa michezo akiwa peke yake huku jua linawaka na hapana kivuli.]





[Maelezo ya picha: Kuna meza mbili na watoto watatu waliokaa katika kila meza. Kuna mabango machache yaliyotundikwa ukutani yenye maandishi. Upande wa kushoto kuna watoto watatu wa kike wakiwa wanatazamana wakiwa na vitabu vilivyofunguliwa mbele yao. Mtoto mmoja wa kike anasema "swali la 2 lilikuwa insha", mtoto mwengine wa kike anagongo la kutembelea. Mtoto mwengine wa kike wa tatu anamuangalia mwalimu ambae amesimama karibu yake akisema "kuna yeyote anayehitaji msaada?" Upande wa kulia kuna watoto wawili wa kiume wakiulizana "Have you finished?" Mtoto wa tatu wa kiume amekaa peke yake anawaza na kujisemea "mimi sielewi". Maneno mengine yote katika maduara ya wasemaji kwenye picha yameandikwa kwa lugha ya Kiswahili.]



[Maelezo ya picha: Kuna meza mbili na watoto watatu waliokaa katika kila meza. Upande wa nyuma kushoto kuna watoto watatu wa kike waliokaa wanatazamana. Mtoto mmoja anaandika, mwengine anazungumza na wa tatu ana gongo la kutembelea kando yake. Kuna mabango machache yenye maandishi yaliyobandikwa ukutani upande wa nyuma. Katika meza ya mbele kuna watoto watatu wa kiume. Mtoto aliyekaa kushoto ni mkubwa kiumbo na anaonekana ni mkubwa pia kiumri kuliko watoto wengine waliopo darasani. Amekaa peke yake na anaonekana mwenye huzuni. Watoto wengine wa kiume wanazungumza na kufanya kazi pamoja.]




[Maelezo ya picha: kuna skuli iliopo ufukweni mwa bahari. nje kuna bango lilioandikwa skuli, kuna wanafunzi wawili waliovaa sare za skuli. Mwanafunzi wa kiume anaonekana akiingia katika eneo la skuli akiwa amevaa mkoba mgongoni kwa mbali upande wa madarasa ya kushoto mtoto wa kike alievaa mkoba anaonekana kuelekea darasani.  Ufukweni mwa bahari kuna kijana alievaa bukta anaonekana kunyoosha mkono ili apokee pesa kutoka kwa mwanamke alievaa shungi. Kati kati yao kuna meza iopangwa samaki. Pembeni kuna mwanamke aliekaa chini akionekana anasafisha samaki, pembeni mwake kuna samaki wengi.]




[Maelezo ya picha; Upande wa kushoto nyuma ya picha kuna skuli na watoto wawili wa kike waliovaa sare za skuli waliosimama mbele ya skuli, na mfanyakazi mmoja au wawili na wanafunzi wapo nje ya skuli. Upande wa mbele wa picha mkono wa kulia kuna watoto watatu wa kike waliochukua ndoo na maji. Wanaangalia upande uliopo skuli.]




[Maelezo ya picha: Upande wa kushoto kuna skuli. Inaonekana kuwa imefungwa. Kuna uzio unaozunguka skuli na mbele yake kuna maji ya tope nyingi. Upande wa kulia kuna nyumba chache na baadhi ya majengo yaliovunjika. Kuna watoto wawili wa kiume na mtoto wa kike anayeandaa chakula mbele ya nyumba. Kuna kizuizi cha barabarani katika moja ya Barabara.]

# Kielelezo nam. 2.1: Picha za sera




[Maelezo ya picha: Slaidi inaonesha picha tatu zilizowekwa moja pembeni ya nyengine. Picha ya kwanza iliyopo kushoto inaonesha Katiba ya Zanzibar. Ina rangi ya kijani iliokoza kwa maandishi ya dhahabu. Juu ya jalada kuna nembo ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, katikati imeandikwa Katiba ya Zanzibar ya 1984 na chini kabisa imeandikwa toleo la 2010. Pembeni ya picha hii kuna picha nyengine ya Sera ya elimu. Sera hio juu ina nembo ya serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, chini ya nembo hio kuna maneno yalioandikwa kwa Kiingereza yanayosema Serikali ya mapinduzi ya Zanzibar, chini yake imeandikwa Wizara ya elimu na mafunzo ya amali. Chini ya maneno hayo kuna picha zilizokusanywa pamoja zinazoonesha majengo ya skuli na wanafunzi wakiwa madarasani. Chini ya picha hio kuna 2006 kuashiria mwaka iliopitishwa sera hio. Pembeni ya picha hio kuna picha nyengine yenye rangi nyeupe juu ikiwa na rangi nyeusi na chini kabisa ina rangi ya buluu na ya kijani. Juu kuna nembo ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na maneno hayo yameandikwa kwa Kiingereza chini ya nembo hio. Chini yake kuna maneno mengine yakiingereza yanayosema Ofisi ya makamo wa pili wa Rais, na chini yake kuna maneno yanayosema sera ya watu wenye ulemavu Zanzibar. Na chini yake kuna 2018 kuashiria mwaka iliopitishwa Sera hio.]

# Nyenzo: 2.2: Sheria na Sera za haki ya elimu Zanzibar

Zanzibar ina idadi ya sheria zilizotungwa ambazo zinahakikisha haki za watoto wote kupata elimu bora, afya na matunzo ya jumla. Ingawa hakuna sera mahususi kuhusu watoto walio nje ya skuli na watoto wenye ulemavu, haki zao zimeainishwa kwa upana katika sheria na sera zilizotajwa hapa chini.

## Kielelezo nam. 2.2a: Katiba ya Zanzibar

| |
|---|
| Katiba ya Zanzibar haielezi moja kwa moja ulinzi wa haki ya elimu. Hata hivyo, Katiba ya Zanzibar inaahidi kwamba:<br>Raia wote ni sawa mbele ya sheria, pia wana majukumu sawa na fursa kwa mujibu wa sheria, kuthaminiwa utu wao na haki nyengine za binaadamu zinaheshimiwa na kuenziwa, uhuru, kutokuwepo upendeleo, uadilifu mbele ya vyombo vya sheria na fursa ya kupata huduma za sheria kupitia mahakama ni haki ya msingi inayopaswa kuheshimiwa.<br>Malengo ya huduma za afya, elimu na utamaduni:<br>Serikali itaelekeza sera zake katika kuhakikisha kwamba kila mtu anapata huduma za kuridhisha za afya, fursa sawa katika upatikanaji wa elimu inayokidhi mahitaji na kwamba utamaduni wa Zanzibar utalindwa, kuimarishwa na kutangazwa. |

## Kielezo nam 2.2b: Sera ya elimu ya Zanzibar 2006

| |
|---|
| Sera iko chini ya mchakato wa kuhakikiwa na kurekebishwa, lakini ya sasa imetaja kauli na mikakati ifuatayo:<br><br>Taarifa za Sera:<br>Elimu mjumuisho itakuzwa ili kuhakikisha kwamba watoto wenye mahitaji maalum wanapata fursa sawa, vikwazo vya kujifunza vitashughulikiwa na mahitaji mbalimbali ya kujifunza yatatimizwa.<br><br>Watoto wenye ulemavu na wengine wenye mahitaji maalum, kwa kadiri inavyowezekana, wataweza kuhudhuria shule iliopo karibu nao ambapo watapata elimu bora pamoja na wenzao wasio na ulemavu/mahitaji maalum.<br><br>Mikakati ya Sera |

- Kutambua watoto wenye mahitaji maalum katika umri mdogo na kutathmini mahitaji yao ya elimu na afya.
- Kupanua na kuimarisha elimu kwa watoto wenye mahitaji maalum.
- Kuunda mbinu za kuweza kuwahusisha na kuwashirikisha watu wenye ulemavu katika masuala yanayohusu maisha yao.
- Kuanzisha vituo maalum vya watoto walio na aina za ulemavu uliokithiri.
- Kuanzisha vituo vya kazi mbalimbali vya walimu.
- Kutetea vilivyo elimu kama haki ya binadamu kwa watoto wenye mahitaji maalum.
- Kuingiza elimu ya mahitaji maalum katika programu za maendeleo ya taaluma ya walimu.
- Kubuni programu maalum kwa wanafunzi wenye uelewa mzito na watoto wenye vipawa.
- Kuanzisha huduma za rufaa.
- Kutoa fursa za ajira kwa watoto wenye mahitaji maalum.
- Kuanzisha uhusiano na ushirikiano imara na Jumuiya za watu wenye ulemavu, Wizara yenye dhamana ya Maendeleo ya Vijana, Ajira, Wanawake na Watoto, Wizara yenye dhamana ya afya, washirika wa maendeleo na jamii kwa ujumla

## Kielelezo nam 2.2c: Sheria ya Watoto nam 6 ya 2011 kifungu cha 11(2)

Mtoto mwenye ulemavu atastahiki uangalizi na ulinzi maalum na atapata fursa ya kufikia na kupata elimu jumuishi na isiyobagua, mafunzo, huduma za afya, huduma za marekebisho, maandalizi ya ajira na fursa za burudani kwa namna itakayomwezesha mtoto kupata mafanikio kamili, ushirikiano wa kijamii na maendeleo ya mtu binafsi, kuhakikisha utu wake na kukuza kujitegemea na ushiriki wake katika jamii.

## Kielelezo nam 2.2d: sera ya watu wenye ulemavu ya mwaka 2018

Sera ya ulemavu imeonyesha uchanganuzi wa hali ya elimu kuhusiana na watu wenye ulemavu. Imetaja zaidi jukumu la Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi lakini haijataja haswa watoto walio nje ya shule. Yafuatayo ni majukumu yaliyotajwa katika sera:

1. Kutayarisha na kutekeleza mitaala ya shule za msingi, sekondari na baada ya sekondari ambayo inasisitiza masuala muhimu ya elimu-mjumuisho.
2. Kutenga wataalamu wa kutosha ili kushiriki katika uandaaji na utekelezaji wa programu za mafunzo ya amali kwa watu wenye ulemavu.
3. Kutoa elimu mjumuisho ilio bora katika ngazi zote.

4. Kusimamia utoaji wa elimu-mjumuisho kwa wasomi wote.
5. Kujengea uwezo juu ya masuala ya ulemavu kwa wazazi, walimu, wanafunzi, wapangaji wa elimu na wadau wengine wa elimu.
6. Kufanya tafiti zinazofaa kuhusu elimu kwa wote wakiwemo watu wenye ulemavu
7. Kutoa mafunzo ya amali kwa watu wenye ulemavu.

## Kielelezo nam. 2.2e: Mkataba wa Umoja wa Mataifa wa Haki za Watu wenye Ulemavu, 2006, Ibara ya 24: Elimu (kama ulivyoridhiwa na Tanzania)

Nchi Wanachama zinatambua haki ya watu wenye ulemavu kupata elimu. Kwa nia ya kutambua haki hii bila ubaguzi na kwa msingi wa fursa sawa, Nchi Wanachama zitahakikisha mfumo wa elimu-mjumuisho katika ngazi zote na kuendeleza kujifunza ikielekezwa kwa:
Ukuzaji kamili wa uwezo wa binadamu na hisia ya utu na kujithamini, na kuimarishwa kwa heshima ya haki za binadamu, uhuru na utofauti wa binadamu;
Ukuzaji wa utu wa watu wenye ulemavu, talanta na ubunifu, pamoja na uwezo wao wa kiakili na wa kimwili, kulingana na uwezo wao;
Kuwawezesha watu wenye ulemavu kushiriki kikamilifu katika jamii huru.

2. Kwa kuitambua haki hii, Nchi wanachama watahakikisha kuwa:
(a) Watu wenye ulemavu hawajatengwa katika mfumo wa elimu kwa sababu ya ulemavu, na kwamba watoto wenye ulemavu hawajatengwa kutoka katika elimu ya msingi ya bure na ya lazima, au kutoka katika elimu ya sekondari, kwa sababu ya ulemavu;
(b) Watu wenye ulemavu wanaweza kupata elimu bora ya msingi na ya sekondari ilio mjumuisho, sawa na wengine katika jamii wanamoishi;
(c) Mazingira stahiki ya mahitaji ya mtu binafsi hutolewa;
(d) Watu wenye ulemavu hupata msaada unaohitajika, ndani ya mfumo wa elimu, ili kuweza kupata elimu yenye ufanisi;
(e) Hatua madhubuti za usaidizi binafsi hutolewa katika mazingira ambayo huongeza maendeleo ya kitaaluma na kijamii, kulingana na lengo la ujumuishaji kamili.

3. Nchi Wanachama zitawawezesha watu wenye ulemavu kujifunza stadi za maisha na maendeleo ya kijamii ili kuwezesha usawa katika kushiriki kikamilifu katika elimu na kama wanajamii. Kwa ajili hiyo, Nchi Wanachama zitachukua hatua zinazofaa, zikiwemo:

(a) Kuwezesha ujifunzaji wa nukta nundu, hati mbadala, hali zilizo mbadala na za kukuza, njia na miundo ya mawasiliano na ujuzi wa kujongea na kujua mazingira, na kuwezesha ushauri na usaidizi rika;
(b) Kuwezesha ujifunzaji wa lugha ya alama na kukuza utambulisho wa usomaji wa matamshi wa jamii ya viziwi;
(c) Kuhakikisha kwamba elimu ya watu, na hasa watoto, wasioona, viziwi au ulemavu wa uziwi na, inatolewa kwa lugha na hali na njia zinazofaa zaidi za mawasiliano kwa mtu binafsi, na katika mazingira ambayo huongeza ukuzaji wa kitaaluma na kijamii.
4. Ili kusaidia kuhakikisha utimilifu wa haki hii, Nchi Wanachama zitachukua hatua zinazofaa kuajiri walimu, wakiwemo walimu wenye ulemavu, waliohitimu katika lugha ya alama na/au nukta nundu, na kutoa mafunzo kwa wataalamu na wafanyakazi wanaofanya kazi katika ngazi zote za elimu. . Mafunzo hayo yatajumuisha kufahamu ulemavu na hali ya matumizi ya njia mbadala na yakukuza, njia na miundo ya mawasiliano, mbinu za elimu na nyenzo za kuwasaidia watu wenye ulemavu.
5. Nchi Wanachama zitahakikisha kwamba watu wenye ulemavu wana uwezo wa kupata elimu ya juu, mafunzo ya amali, elimu ya watu wazima na kuendelea kujifunza bila ubaguzi na kwa usawa kama watu wengine. Kwa maana hii, Nchi Wanachama zitahakikisha kwamba mazingira stahiki yanapatikana kwa watu wenye ulemavu.

## Kielelezo nam 2.2e: Mkataba wa haki za mtoto, Ibara 23 (kama ulivyoridhiwa na Tanzania)

Nchi Wanachama zinatambua kwamba mtoto mwenye ulemavu wa kimwili au kiakili anapaswa kufurahia maisha kamili na yenye heshima, katika hali zinazohakikisha utu, kukuza kujitegemea na kuwezesha ushiriki wa mtoto katika jamii.
Nchi Wanachama zinatambua haki ya mtoto mwenye ulemavu kupata matunzo maalum na zitahimiza na kuhakikisha kuongeza msaada, kwa kutegemea rasilimali zilizopo, kwa mtoto anayestahiki na wale wanaohusika na malezi yake, msaada ambao maombi yanafanywa na ambayo ni kulingana na hali ya mtoto na hali ya wazazi au watu wengine wanaomtunza mtoto huyo.
Kwa kutambua mahitaji maalum ya mtoto mwenye ulemavu, msaada unaotolewa kwa mujibu wa aya ya 2 ya kifungu hiki utatolewa bila malipo, pale itakapowezekana, kwa kuzingatia rasilimali za kifedha za wazazi au watu wengine wanaomtunza mtoto, na itaundwa ili kuhakikisha kwamba mtoto mwenye ulemavu anafikia na kupata elimu, mafunzo, huduma za afya,

huduma za marekebisho, maandalizi ya ajira na fursa za burudani kwa njia ambayo itamwezesha mtoto kufikia kikamilifu ushirikiano wa kijamii na maendeleo ya mtu binafsi, ikiwemo maendeleo yake ya kitamaduni na kidini. Nchi Wanachama, kwa nia ya ushirikiano wa kimataifa, zitakuza ubadilishanaji wa taarifa zinazofaa katika uwanja wa kinga ya huduma ya afya na matibabu, kisaikolojia na matibabu ya watoto wenye ulemavu, ikiwemo usambazaji na upatikanaji wa taarifa kuhusu njia za marekebisho; elimu na huduma za ufundi, kwa lengo la kuwezesha Nchi Wanachama kuboresha uwezo na ujuzi wao na kupanua uzoefu wao katika maeneo haya. Kwa muktadha huu, angalizo maalum litazingatiwa juu ya mahitaji ya nchi zinazoendelea.

## Kielelezo nam. 3.1: Kadi za almasi 9 – Vikwazo vinavyowazuia wanafunzi kwenda skuli

Kadi hizi zikatwe kabla ya kupewa washiriki.

| | | |
|---|---|---|
| **Mtazamo kuhusu umri** | **Mtazamo kuhusu tabaka/hadhi ya kijamii na kiuchumi** | **Mgogoro** |
| **Mtazamo kuhusu Ulemavu** | **Mtazamo kuhusu Ukabila** | **Mtazamo kuhusu Jinsia** |
| **Afya** | **Lugha** | **Uhamiaji** |
| **Umasikini** | **Mtazamo kuhusu Dini** | **Majanga** |
| | kadi ambazo hazijaandikwa kwa ajili ya washiriki kuandika maoni yao kuhusu vikwazo. | |
| | | |

# Nyenzo 3.2: Visa mafunzo vinavyowahusu wanafunzi walio nje ya skuli

1.**Salma** anatumia kitimwendo. Anataka kuhudhuria skuli jirani na marafiki zake anaoishi nao karibu na kwao. Skuli haina miundombinu ya kuwezesha kitimwendo kuingia ndani ya skuli, kwa hivyo binamu yake ambae alikuwa hajaajiriwa alifuatana nae ili amuinue kwenye ngazi na kumfikisha kwenye njia ya kuelekea mlangoni. Binamu yake sasa ameajiriwa na hawezi kufuatana nae tena. Uongozi wa skuli unasema kwamba Salmo hawezi kuendelea kwenda skuli bila ya msaidizi. Salma amebaki nyumbani tangu ulipotoka uamuzi huo.

2. **Daudi** ana tabia isiyopendeza na tatizo la kudhibiti hisia zake. Alipokuwa anakwenda skuli aliweza kutulia kwa dakika 15 tu na karibu kila mara alikuwa katika matatizo darasani. Alikuwa akifanya fujo, tabia ambayo humtia matatizoni zaidi na mara nyingi walimu wake humfukuza kutoka darasani. Daudi ameamua kutokwenda skuli. Hivi sasa haendi tena skuli badala yake hutumia muda mwingi akizurura mjini na vijana waliomzidi umri na hujikuta kwenye mgogoro na wafanyabiashara na polisi.

3. **Tawfiiq** ana tatizo la uoni hafifu na ulemavu wa akili. Wazazi wake wanaona aibu kuwa na mtoto kama yeye. Wanaishi mbali na skuli kwa hivyo huwasaidia wazazi wake kuuza mboga katika soko jirani na hajawahi kuandikishwa skuli.

4. **Hassan** ana umri wa miaka 11 akiwa katika shule ya msingi. Ana tatizo na somo la hesabati; hafahamu akipewa kazi na mara nyingi hupata majibu yasio sahihi. Mwalimu humpiga anapokosea kwa hivyo Hassan kaamua kutohudhuria vipindi vya somo la Hesabati. Wiki iliyopita Hassan aliamua kuacha kabisa skuli.

5. **Amina** hajui kusoma na aliacha skuli akiwa na umri wa miaka 9. Alilazimishwa kuolewa alipofika umri wa miaka 14. Familia ya Amina ni masikini sana, waliamua kumuoza ili familia ipate fedha na kujikimu. Amina bado anaishi na familia yake.

6. **Faraji** ni mtoto wa kiume mwenye umri wa miaka kumi anayeishi katika kijiji cha Cheju Kusini mwa Zanzibar. Familia yake inamiliki ng'ombe na yeye ana jukumu la kuchunga mifugo hiyo. Wakati wa kiangazi familia huhamia katika vijiji jirani kutafuta maji na malisho. Faraji hajawahi kuandikishwa skuli.

7. **Shakira** ana umri wa miaka 14 akiwa darasa la saba. Aliacha kwenda skuli wakati wa kipindi cha mitihani. Uongozi wa skuli ulipoitembelea familia yake, baada ya kufanya mitihani yake miwili, aligoma kwenda skuli na familia yake haikusema chochote kumsihi abadili msimamo wake. Baadaye, alipozungumza na marafiki zake alisema kwamba skuli haina umuhimu, ameamua aolewe, na wazazi wake walimuoza kwa bwana mmoja mtu mzima.

8. **Halima** ana umri wa miaka 12. Anaishi na familia yake yenye watoto tisa katika vyumba viwili vidogo. Hakuna yeyote katika familia yao ambaye amewahi kusoma skuli. Mama yake anatembea umbali wa kilomita 6 kila siku kukusanya mabaki ya vyakula kutoka mahotelini katika mji mwengine ili kuongezea chakula cha familia. Wakati huo huo Halima hutumwa akauze karanga katika sehemu ya michezo ya kubahatisha karibu na kwao.

9. **Omar** ana umri wa miaka 10. Alifurahi sana alipoanza skuli miaka michache iliopita, lakini furaha yake ilidumu kwa muda mfupi. Walimu wake hawakuweza kumvumilia. Ni mtundu sana na walimu wake wanadhani ana tabia mbaya na ni mgomvi. Mara nyingi pia hugombana na wazazi wake. Wazazi wake wamejaribu kutafuta suluhu ya tatizo lake bila mafanikio. Walijisikia kukata tamaa, kuhuzunika na kughadhibika pia, wakati mwengine humtolea maneno makali, kumuadhibu au hata kuacha kuzungumza naye. Marafiki zake viwanjani na mtaani humchokoza na hukataa kucheza nae; humwambia 'anaharibu' michezo yao. Omar ameacha kwenda skuli.

10. **Nawal** ana umri wa miaka 10. Alilazimika kuishi na shangazi yake baada ya wazazi wake kufariki kwenye ajali ya barabarani. Nawal alipomuomba shangazi yake amuandikishe skuli aliwmbiwa "unapaswa kufanya kazi kulipia chakula unachokula" kwa hivyo akawa mtumishi katika nyumba ya shangazi yake. Wakati mwengine shangazi yake humpiga.

11. **Mohammed** alizaliwa katika kijiji kimoja cha wilaya ya Chakechake. Mohammed alizaliwa akiwa haoni kabisa. Alipofika umri wa miaka 6 alitamani kujifunza Qur'an kama wenzake. Alipofikisha umri wa miaka 13 aliamua kwenda mahali karibu na chuo cha Qur'an ambapo alikaa na kuwasikiliza wanafunzi wakisoma Qur'an pamoja na walimu wakisomesha. Kwa njia hii Mohammed alijifunza sura nne za Qur'an. Alimkabili mwalimu na kumsomea sura nne alizohifadhi. Ijapokuwa mwalimu alishangazwa, lakini hakuwa tayari kumpokea Mohammed kuwa mwanafunzi wake, kwa kuwa Mohammed hakidhi vigezo vya kuwa mwanafunzi katika chuo hicho.

12. **Sahra** ana umri wa miaka 12 kutoka sehemu ya Kusini mwa Zanzibar. Alihama akifuatana na mama yake pamoja na ndugu zake, wakati ulipotokea uchafuzi wa maji ya bahari katika kijiji chao miaka michache iliyopita na amekosa miaka kadhaa ya kuwa skuli. Sahra hivi sasa anaishi katika hali mbaya katika makaazi ya muda na familia yake. Sahra alisaidiwa kujiunga na programu ya elimu iliofadhiliwa na Jumuiya Isiyo ya Kiserikali kwa ajili ya watu waliokoseshwa makazi kutoka Kusini, lakini alipata shida ya kupata utulivu na alijiona umri wake ni mkubwa kujiunga na masomo hayo. Hatimaye aliamua kuacha skuli ili kumsaidia mama yake kutafuta fedha kwa ajili ya familia.

# Kielelezo nam. 3.3: Mikakati na suluhisho la kuwatafuta na kuwatambua wanafunzi walio nje ya skuli

| Wapo WAPI? | Tutumie mbinu GANI ili kuwatambua na kuwapata? |
|---|---|
| **NANI katika jamii yenu anaweza kutusaidia kuwatafuta?** | **Tunaweza kukabiliwa na changamoto zipi na VIPI tutazitatua?** |

## Kielelezo nam. 4.1: Maelezo ya video ya 'Uhamaji jumuishi' iliyoandaliwa na EENET: Kwa nini uhamaji ni jambo linalotiliwa maanani katika elimu mjumuisho?

Watoto wote hupitia vipindi tofauti vya uhamaji katika maisha yao ya kutafuta elimu – kutoka nyumbani na kujiunga kwa mara ya kwanza katika kituo cha maandalizi au skuli, mpaka siku yao ya mwisho katika maisha ya skuli, chuo au Chuo Kikuu, na baadae kuanza kazi.

Kuhamia skuli mpya au darasa jengine kunaweza kuwa ni jambo la kufurahisha, kutia hofu, kuchanganya kimawazo au kutoridhishwa.

Inaweza kuwa ni jambo ambalo halikuwa tayari kupokelewa kwa mtoto na familia yake.

> 'Ni hatua ya kutia wasiwasi pale mtoto anapoanza safari yake ya kuelekea skuli. Kundi jipya la watoto huundwa; huku wakijaribu kuonesha tabia zao. Ni hatua ngumu pale watoto wanapojaribu kuzoeana katika kundi lao jipya'. *(Olha Serova, Mother of Artem, Pre-school No. 2, "Romashka", Mykolayivka)*

Kila wakati mtoto anapojiunga na mazingira mapya ya elimu au darasa inachukuwa muda kwao kuzoea, na kwa mwalimu kujua mahitaji yao binafsi.

Hii ina maana wakati wa kipindi cha uhamaji kuna hatari ya kwamba ushiriki na mchakato wao wa kujifunza utaingiliwa kati, hasa kwa watoto ambao wanahitaji usaidizi wa ziada.

> 'Ilia hivi sasa amepata utulivu katika skuli yake ya maandalizi. Bila ya shaka, kama mama, nina wasiwasi kuhusu hatua nyengine, itakuwaje kesho yake, na nafahamu kuwa hatua nyengine ni skuli ya msingi. Bila ya shaka ni lazima iwe skuli jumuishi. Ndio, nina hofu. Lakini skuli za namna hiyo zinapatikana kule Kharkiv. Wana elimu ya kutosha na uzoefu na wanawapokea watoto wenye ulemavu. Kwa hivyo natumai Ilia atakapohitimu kutoka ngazi ya maandalizi tutapata skuli muwafaka ambayo ni jumuishi ambapo tutakaribishwa na kupokelewa'.
> *(Nina Arsentieva, Mother of Illia, Community Pre-school No 74, Kharkiv City).*

Mfumo wa elimu mjumuisho unapaswa kuhakikisha kwamba kila kipindi cha uhamaji kimeratibiwa vyema na kuwezeshwa, ikihusisha ushirikishwaji kamili wa wazazi na walezi, kwa hivyo hakuna mtoto anayeachwa nje ya mfumo wa elimu wakati wa kipindi hiki kigumu.

## Uhamaji jumuishi wa elimu huanzia nyumbani

Wazazi na walezi wana ushawishi mkubwa katika makuzi na mchakato wa kujifunza wa mtoto wao, kabla hata hawajazaliwa.

Husaidia ukuaji wa mtoto wao kijamii, kimwili, kiakili, ubunifu na kihisia, jambo ambalo humsaidia mtoto kuwa muhimilivu na mwenye fikra huru.

Wazazi na walezi hulifanikisha vyema jambo hili kupitia michezo.

Shughuli zinazoambatana na michezo huwasaidia wazazi na walezi kubaini iwapo mtoto wao ana changamoto fulani.

Kujenga msingi mapema wa makuzi na kujifunza nyumbani husaidia kufanya mchakato wa uhamaji kwenda katika mazingira ya mwanzo ya elimu kuwa hauna usumbufu mkubwa.

Watoto hujifunza na kutumia aina mbalimbali za ujuzi nyumbani ambao watahitaji kuutumia watakapokwenda  skuli.

## Muendelezo wa usaidizi wa uhamaji

Uhamaji jumuishi ni mchakato unaotokea pale wanafunzi wanapoondoka nyumbani kuelekea katika mazingira ya mwanzo ya kujifunza, au kwenda darasa jipya au mazingira mapya, ni mchakato mwepesi kwao, familia zao, na walimu.

Hakuna mabadiliko yasiotarajiwa au mshituko.


Kuna wasiwasi mdogo, na watoto huendelea kupokea usaidizi wanaouhitaji ili kuwasaidia kuimarisha kile ambacho tayari wanajua kuwa wanaweza kufanya.

Utachangiaje uendelezaji wa usaidizi huu?

## Kielelezo nam. 4.2: Nini maana ya uhamaji katika taasisi za elimu?




[Maelezo ya picha: Upande wa juu kushoto, kuna jengo lililoandikwa ‘skuli ya msingi’. Mtoto wa kike anatembea kuelekea upande wa skuli akiwa ameshika fimbo nyeupe. Kuliani kuna jengo lililoandikwa ‘skuli ya sekondari’. Mtoto yuleyule akionekana mkubwa zaidi anatembea akitokea skuli ya msingi kuelekea sekondari akiwa ameshika fimbo nyeupe. Chini kuna jengo limeandikwa ‘Chuo Kikuu’. Kijana wa kike anatembea kutoka sekondari akielekea Chuo Kikuu akiwa ameshika fimbo nyeupe].




[Maelezo ya picha: Mtoto wa kiume aliyevaa sare ya skuli, akiwa amebeba begi anapanda ngazi. Maneneo 'Dugsi Hare' yameandikwa juu ya ngazi. Watoto watatu wamesimama chini ya ngazi. Watoto hao ni pamoja na mtoto mmoja wa kiume aliyevaa shuka iliyofungwa kiunoni akimuangalia mtoto mwengine wa kiume, mtoto mwengine wa kike aliyembeba mtoto mgongoni akionekana mwenye huzuni na mtoto mwengine wa kiume aliyevaa miwani myeusi, ameshika fimbo akiangalia upande mwengine. Maneno 'Dugsi Hoose' yameandikwa chini ya ngazi.]

# Kielelezo nam. 4.3: Walichosema wanafunzi kuhusu uhamaji

Sioni njia hapa au hamna njia inayopitika kwenda katika skuli yangu mpya.

Nina wasiwasi sitopata marafiki wapya au kuweza kushiriki ipasayo katika mambo ya skuli.

Wazazi wangu hawajihusishi sana na mimi sasa hivi tangu niingie madarasa ya juu, lakini bado ningependa wazungumze na walimu wangu ninapokuwa na matatizo

Sikuwahi kuona jinsi ilivyo ndani skuli yangu mpya siku niliyokwenda kuanza muhula wa kwanza. Nilikuwa naogopa.



Ratiba mpya inanichanganya. Natakiwa niende wapi na saa ngapi? Nagombwa kwa kuchelewa.

Kila mtu anahisi nimeshakuwa mkubwa na ninaweza kuzoea katika skuli yangu mpya. Bado naogopa na najisikia kuchanganyikiwa.

Skuli ipo mtaa mwengine – jambo hilo linanitisha.

Nimeingia matatani kwa kuonekana jeuri kwa mwalimu wangu mpya kwa sababu sifahamu anachotaka nifanye.

Ni ngumu kufaulu kwenda ngazi nyengine. Mtihani haujazingatia mahitaji yangu.


Sijazoea kuwa mbali na wazazi wangu siku nzima.

Walimu katika skuli yangu niliotoka walipanga jinsi ya kunisaidia katika baadhi ya masomo. Skuli yangu mpya haitambui hili. Mipango yote ya kusaidiwa inabidi inabidi ifikiriwe upya. Natamani mwalimu wangu wa zamani angehusishwa.

Walimu wanafanya mambo tofauti na nilivyozoea katika skuli hii. Wana mbinu tofauti za kufundishia. Nashindwa kujua matarajio yao.

Nataka kujiunga na chuo cha mafunzo ya amali. Sijui vyuo gani ni jumuishi kwa wanafunzi wenye ulemavu. Pia hakuna mtu yeyote anayejua katika skuli yangu.

# Kielelezo nam. 5.2a: uhamaji jumuishi huanzia nyumbani



[Maeleo ya picha: Picha inaonesha kikundi cha wanafamilia wakiwa katikati na majengo manne yaliyopo katika kila pembe, pakiwa na njia na mishale iliyounganisha majengo na familia. Familia inajumuisha mtoto wa kike, mtoto mkubwa wa kike na mtoto mkubwa wa kiume, mzee aliyeshika fimbo ya kutembelea, mwanamke na mwanamme. Maneno ‘familia na nyumbani’ yameandikwa chini ya kikundi cha familia. Upande wa juu kushoto, kuna jengo lililoandikwa ‘kituo cha maandalizi’. Mtoto mdogo wa kike akiwa ameshika mkono wa mtoto mkubwa wa kike wanatembea kuelekea ‘kituo cha maandalizi’. Kuna mshale uliopinda kutoka kituo cha maandalizi kuelekea upande wa juu kulia ambako kuna jenge lililoandikwa ‘skuli ya msingi’. Picha ile ile yam toto wa kike ambae anaonekana mkubwa sasa anatembea kutoka katika familia yake kwenda skuli ya msingi. Kuna mshale uliopinda kutoka skuli ya msingi kwenda chini upande wa kulia ambako kuna jengo lililoandikwa ‘skuli ya sekondari’. Picha yam toto yule yule wa kike akionekana mkubwa sasa anatembea kutoka kwenye familia yake kwenda skuli ya sekondari. Mwisho, kuna mshale uliopinda ukielekea pembe ya chini kushoto ambako kuna jengo lililoandikwa ‘chuo kikuu’. Mwanamke anatembea kutoka katika familia yake kwenda chuo kikuu.]


## Kielelezo nam. 5.2b: Seti ya picha tatu za mikakati



[Maelezo ya picha: Kuna watoto watatu ambao wanacheza nje. Watoto wa kiume wawili na wa kike mmoja. Mtoto mkubwa wa kiume ambae yupo upande wa kushoto anaonekana kama anapiga kwa mguu. Kuna mpira wa miguu mbele yake. Mtoto wa kiume aliyevaa fulana ya rangi ya njano ambae yupo upande wa kulia ambae anatembea kwenda kwenye mpira; kashika fimbo ndefu. Mtoto wa kike amekaa mbali kidogo upande wa kushoto, anapiga makofi na kumhamasisha. Nyuma yao kuna mwanamme na mwanamke ambao wanaangalia na kutabasamu.]


Inclusive School

[Maelezo ya picha: Kuna watu watatu wamesimama nje wakizungumza. Mwanamke mmoja anagawa baadhi ya vipeperushi vya rangi ya njano kwa wengine. Karibu na hapo  kuna mwanamme anabandika kipeperushi cha rangi ya njano nje ya jengo kilichoandikwa 'skuli jumuishi'. Nyuma ya picha kuna mwanamme mwengine anagawa vipeperushi kwa watu wawili ambao wanakaa na kuzungumza. Nyuma kabisa kuna mbuzi na nyumba chache za kijiji na mwanamme pamoja na mtoto wa kiume wakilima bustani.]


SKULI
Uandikishaji

[Maelezo ya picha: Watu wengi wamekusanyika nje, mbele ya jengo la skuli. Upande wa kushoto kuna mwanamke aliyekaa kwenye dawati lenye maandishi ‘uandikishaji’ pembeni. Kuna wanawake wawili na watoto wawili waliosimama mbele ya dawati. Upande wa nyuma ya picha, mbele ya skuli, watoto wawili wa kiume wanaingiza meza darasani. Upande wa kushoto nyuma ya dawati, kuna watoto watatu wa kiume, akiwemo mmoja mwenye gongo la kutembelea wanacheza mpira wa miguu. Upande wa kulia, baadhi ya watu wamekusanyika kwenye viti chini ya shamiana wanamsikiliza mwanamke anayezungumza.]

# Kielelezo nam. 5.3a: Mambo yanayoathiri uhamaji kabla ya kujiunga na skuli

**Kikundi cha 1, watajadili kuhusu usingizi.**

Chukua karatasi ya flipchati na chora mchoro wa kawaida wa mtoto aliyelala katikati. Halafu jadilini yafuatayo na muandike maelezo kwenye flipchati:

Jambo gani husababisha watoto katika skuli yenu kutokupata usingizi wa kutosha?

- Vipi ukosefu wa usingizi huathiri ujumuishwaji wa watoto katika elimu?
- Vipi usingizi husaidia ujumuishwaji wa watoto katika elimu?
- Nini kifanyike ili kuhakikisha wanapata usingizi wa kutosha?

**Kikundi cha 2, watajadili kuhusu kifungua kinywa.**

Chukua karatasi ya flipchati na chora mchoro wa kawaida wa mtoto anayekula kifungua kinywa katikati, au japo picha ya bakuli na kijiko. Halafu jadilini maswali yafuatayo na Andika maelezo kwenye flipchati:

- Kwa nini watoto katika skuli yako inawezekana wasipate kifungua kinywa?
- Vipi ukosefu wa kifungua kinywa huathiri ujumuishwaji wa watoto katika elimu?
- Vipi upatikanaji wa kifungua kinywa husaidia ujumuishwaji wa watoto katika elimu?
- Nini kifanyike ili kuhakikisha watoto wanapata chakula kabla hawajaondoka kwenda skuli?

**Kikundi cha 3, watajadili kuhusu majukumu.**

Chukua karatasi ya flipchati na chora mchoro wa kawaida wa mtoto akifanya kazi za nyumbani. Halafu jadilini maswali yafuatayo na andika maelezo kwenye flipchati:

- Kazi watoto katika jamii yenu hufanya na kwa nini hufanya kazi hizo?
- Vipi kazi za nyumbani, shamba au katika jamii huwa na athari hasi kwa elimu ya mtoto?
- Vipi huweza kuwanufaisha watoto katika elimu?
- Nini kifanyike ili kuhakikisha kwamba kazi za nyumbani haziathiri ujumuishwaji wa watoto katika elimu?

# Kielelezo nam. 5.3b: Maelezo ya video ya 'Kabla ya kufika skuli' iliyoandaliwa na EENET

## Kabla ya kufika skuli

Kila mtoto ana haki ya kubata elimu bora, inayotolewa katika mazingira jumuishi.

Kinachotokea ndani ya skuli kinaweza kumfanya mtoto ajisikie kuwa amejumuishwa au ametengwa.

Lakini matatizo ya kushiriki katika elimu bora huanza kabla mtoto hajafika katika geti la skuli.

## Harakati nyingi mwanzo wa siku

Kuanzia muda ambao mtoto anaamka asubuhi anaweza kukabiliwa na changamoto ambazo zitaathiri ujumuishwaji wake katika elimu.

Watoto wengi, tangu wa kiwa na umri mdogo, husaidia majukumu ya nyumbani – mara nyingi asubuhi kabla hawajaondoka kwenda skuli.

> "Ninachokifanya asubuhi, naamka asubuhi nafyagia na kupiga kudeki sakafu, na tunapika".

Kwa kufanya kazi za nyumbani, watoto husaidia familia, na hujijengea ujuzi na kutambua majukumu.

Lakini majukumu pia yanaweza kuwa kikwazo kwa elimu ya mtoto.

Mitazamo ya kimila kuhusu majukumu ya wanawake na wanaume humaanisha kwamba watoto wa kike mara nyingi hufanya kazi nyingi za nyumbani kuliko watoto wa kiume, nah ii inaweza kuathiri ujumuishwaji wa mtoto wa kike katika elimu.

Bila ya shaka, watoto wa kiume nao hufanya kazi kusaidia familia ambayo yanaweza kuathiri ushiriki wao katika elimu, kama vile kushughulikia mifugo au kufanya kazi ili kupata fedha.

> “Kuhusu suala la jinsia katika skuli yetu, tunapigania fursa sawa, lakini hilo halitutegemi sisi peke yetu. Inategemea pia wazazi. Wazazi, hasa wa watoto wenye ulemavu, mara nyingi huwa hawana uwelewa sawa na huwapa kipaumbele watoto wa kiume kuliko wa kike”.

Kufanya kazi asubuhi kunaweza kusababisha watoto wa kike na wa kiume wachelewe skuli. Wanaweza kuingia matatani kwa jambo hili, ambayo yanaweza kupelekea hatimae kuacha skuli.

Kufanya kazi nyingi pia kunaweza kuwafanya watoto wachoke sana na washindwe kuwa makini na kujifunza ipasavyo.

### Kitu gani ufanye?

Unaweza kuzungumza na watoto darasani kwako au skuli ili kujua kuhusu maisha yao ya nyumbani. Unaweza kuwasaidia kuweka uwiano baina ya majukumu yao ya nyumbani na skuli.

Unaweza kukutana na wazazi ili kujadiliana nao kuhusu athari za majukumu wanayopewa watoto katika elimu. Mnaweza kushirikiana kuratibu upunguzaji wa majukumu hayo.

Mnaweza kuwa na mjadala mpana kuhusu haki za elimu kwa mtoto wa kike, ambayo nchi yako imeridhia kwa kusaini mikataba mbalimbali ya kimataifa.

## Kifungua kinywa

Kifungua kinywa ni mlo muhimu sana kwa watoto.

Kwa bahati mbaya, duniani kote, mamilioni ya watoto wanakwenda skuli hawajala. Hii inaweza kuathiri uwezo wao wa kujifunza – ni vigumu kuwa makini wakati una njaa.

Kuifanya elimu iwe jumuishi huhusisha pia kuhakikisha kwamba watoto hawana njaa.

### Kitu gani ufanye?

> “Programu za utoaji wa chakula katika skuli ni muhimu mno kwa sababu huwahamasisha watoto kuhudhiria skuli ambapo ni sehemu pekee wanayopata chakula. Kwa hivyo ni mbinu nzuri ya kuhamasisha mahudhurio ya wanafunzi wanaotoka katika jamii masikini sana”.

Unaweza kuwachunguza watoto kubaini ni nani anapata tabu ya kufahamu somo kwa sababu ana njaa.

Unaweza kuzungumza na watoto na wazazi wao ili kujua zaidi kuhusu hali zao na kufikiria suluhisho la kuwasaidia.

Unaweza kuishauri skuli yako kuanzisha au kutekeleza klabu ya kifungua kinywa, ili watoto wapate chakula cha bure kabla hawajaanza masomo.

Jumuiya za kijamii au makampuni ya biashara ya eneo hilo yanaweza kusaidia.

Unaweza pia kutafuta taasisi iliyopo katika eneo hilo ambayo inajishughulisha na kuwatafutia watu njia za kujipatia kipato, na kuwashauri washirikiane na wazazi wa skuli yako.

Unaweza pia kusaidia kuanzisha au kusimamia shamba la skuli.

Watoto watajifunza kuhusu mimea, kuotesha mimea ya chakula, na jinsi ya kuhifadhi mazingira wakati wanaotesha mimea ya chakula kwa ajili ya kifungua kinywa na chakula cha mchana.

# Kitini nam. 6.1: Kutumia sera kushawishi mabadiliko

## Igizo: Mkutano wa Kamati ya Elimu ya Kijiji ambayo Jumuiya ya Watu wenye Ulemavu ya Kijiji imeomba kushiriki

### Hali halisi:

Uchafuzi wa Maji ya Bahari kusini mwa Zanzibar. imepelekea watu kutofanya shughuli za uvuvi kwa kwa kipindi kirefu, jambo ambalo limeathiri familia nyingi ambazo sasa zinapambana sana kujikimu. Madhara ya uchafuzi huo yamesababisha familia nyingi kuhamia katikati ya mji wa Zanzibar, ambako kuna msaada bora na huenda wakapata fursa ya kazi mjini. Sasa wanakaa katika sehemu moja maalum ya mji, kwenye majengo na nyumba za zamani ambazo zimekuwa hazitumiki kwa muda mrefu kwa sababu si salama wala stahiki kwa makazi.

Skuli mbili zilizoko karibu na eneo hilo zinapata changamoto kubwa kuwahudumia wanafunzi, kwani familia hizo mpya zinataka watoto wao wapate elimu katika skuli hizo. Hata hivyo, skuli hizo tayari zinakabiliwa na uhaba wa fedha. Watoto watano kati ya wanaotaka kujiunga na skuli kutoka familia hizo mpya wana ulemavu.

Jamii iliyopo katika eneo hilo ni masikini mno na watoto wengi wanaohudhuria katika skuli hizi wanatoka katika familia hizi masikini ambazo zina hali ngumu sana. Kamati ya Elimu ya Kijiji inahisi kwamba skuli hizi tayari zipo katika shinikizo kubwa na haziwezi kumudu wimbi la watoto waliopo, hasa watoto wenye ulemavu. Wanahisi kwamba jukumu lao ni kwa watoto kutoka katika familia za wilaya hiyo waliopo kwa miaka mingi na sio kwa watoto wa familia za mpy. Baadhi ya watoto kutoka katika familia za hizo wamekubaliwa skuli lakini walipata elimu kidogo tu huko walikotoka kwa hivyo wamekuwa wanapata shida kushiriki kikamilifu katika masomo na kwenda sambamba na wenzao darasani. Walimu wengi wapo kwenye shinikizo kubwa kutokana na kuzidiwa na idadi kubwa ya wanafunzi madarasani na hawajui wawasaidie vipi wanafunzi hawa. Kuna mvutano mkubwa katika jamii kuhusu jambo hili. Jumuiya ya Watu wenye Ulemavu imeiomba Kamati hiyo iwapo inaweza kupewa fursa ya kuhutubia katika kikao kwa sababu wana wasiwasi mno na hali inayoendelea. Kwa sababu ni jambo muhimu katika jamii, Kamati imeridhia

kwamba watu kutoka katika jamii jirani na hata familia mpya wanaweza kuhudhuria kusikiliza kitakachojadiliwa.

## Waigizaji:

- **Wajumbe watatu au wanne wa Jumuiya ya Watu wenye Ulemavu:** Wajumbe walijadili mikakati yao na walikubaliana kwamba watawaonesha wajumbe wa Kamati ni jinsi gani haki ya elimu ya watoto hawa wenye ulemavu inakiukwa – kufanikisha hili watatumia Katiba ya Zanzibar na Mkataba wa Kimataifa wa Haki za Watu wenye Ulemavu (CRPD) ambao Zanzibar imeridhia.

  **Mwenyekiti wa Kamati ya Elimu ya Kijiji:** Mwenyekiti wa Kamati ni mpya na anaamini kuwa jukumu la msingi la Kamati ni kwa watoto wanaotoka katika familia zinazotokea katika wilaya ya Mjini kwa miaka mingi. Ana wasiwasi mkubwa akitaka kujijengea taswira nzuri. Haijui vizuri katiba ya Zanzibar au CRPD.

- **Makamo Mwenyekiti wa Kamati ya Elimu ya Kijiji:** Makamo Mwenyekiti ni mwalimu wa zamani na anaamini kuwa haki za walimu ni muhimu zaidi kuliko chochote. Anasema kwamba sera sio muhimu, cha kutiliwa maanani ni kuwa walimu wameelemewa na mzigo wa idadi kubwa ya wanafunzi na wanapokea malipo duni na uwepo wa watoto hawa skuli utawaongezea shinikizo zaidi.

- **Mzee kutoka msikiti wa eneo ambalo familia nyingi kutoka katika Familia mpya huswali:** Mzee huyu ana wasiwasi mkubwa kuhusu hali inayoendelea kwa sababu anafahamu wasiwasi wa wazazi kutoka katika familia mpya na anatamani lipatikane suluhisho. Anaamini kuwa sera ni muhimu na angependa Kamati ijadili jinsi ya kupata suluhisho la tatizo hilo.

- **Mwakilishi wa wazazi wa ambao watoto wao wamekuwa wakisoma skuli hiyo kwa muda:** Mzazi huyu alichukua juhudi kubwa kuhakikisha kuwa watoto wake wanahudhuria skuli akiwa na hofu kuhusu maisha yao ya baadae. Anaamini kwamba skuli haiwezi kuwasaidia watoto hawa na kwamba familia hizo za kusini zirudi kwao – skuli hizi haziwezi kubeba jukumu la kuwasomesha kwa kuwa skuli za Mjini zimelemewa.

- **Wanajamii waliotokea kusini mwa Zanzibar :** Mtu yeyote kutoka katika wakaazi wa asili wa Mjini na wageni wanaruhusiwa kusikiliza kwa sababu kikao hiki ni muhimu. Wanaruhusiwa kuuliza maswali.

**Maswali kwa ajili ya majadiliano:**

- Kwa kiasi gani utumiaji wa sera ulisaidia katika kujadili tatizo la watoto wapya katika kikao cha Kamati?
    - Kama ulisaidia, sera hizo zilisaidia vipi?
    - Kama sera hazikusaidia, kwa nini unasema hivyo?
- Je! Hii inaweza kutokea katika maisha halisi?
- Kuna suluhishi lolote muwafaka ambalo lilipatikana kufuatia mjadala ambalo litaweza kusaidia watoto wakimbizi kupokelwa skuli na pia kuwasaidia wale watoto ambao tayari wapo skuli?
- Kuna tafakuri zozote nyengine kutoka katika igizo ambazo zingeweza kuisaidia Jumuiya ya Watu wenye Ulemavu kuzisaidia skuli katika suala la uhamaji jumuishi?

# Kielelezo nam. 6.2a: Simulizi ya Amina

## Amina, ana umri miaka 15

Amina anatarajia kujiunga na skuli ya sekondari. Ana ulemavu wa kupooza ubongo (Mtindio wa Ubongo). Analazimika kutumia kitimwendo na akizungumza ni vigumu kumuelewa. Wazazi wa Amina, wanafunzi wenzake na walimu wote wanaweza kuwasiliana nae na kumfahamu.

Amina ni hodari na ana malengo. Katika skuli yake anayosoma sasa hivi marekebisho yamefanyika kumuwezesha kusoma.

Baada ya kukutana na uongozi wa skuli ya sekondari kujadili mahitaji ya Amina, mwalimu anaehusika na usajili alimfanyia usaili Amina na kudai kwamba ana shida pia ya kujifunza. Alikataa kumsajili akidhani kwamba hatoweza kumudu masomo ipasavyo. Pia anasema kwamba ijapokuwa huduma nyingi za skuli zinafikika na kitimwendo, hatoweza kusoma baadhi ya msomo ya msingi kwa kuwa madarasa yanakofundishwa masomo hayo hayafikiki.

### Jadili

- Ni yepi mahitaji ya Amina?
- Mbinu zipi zinaweza kusaidia kukidhi mahitaji hayo?
- Uongozi wa skuli/kamati ya elimu mjumuisho ya skuli ifanye nini?
- Kwa njia gani Jumuiya ya Watu wenye Ulemavu inaweza kusaidia kwa ufanisi uhamaji wa mtoto?

# Kielelezo nam. 6.2b: Simulizi ya Yasmin

## Yasmin, ana umri wa miaka 9

Mama yake Yasmin anasema, ulezi wa Yasmin ulikuwa mgumu kwa kuwa alikuwa analia muda wote na alikuwa hawezi kutulia. 'Alikuwa mwanangu wa kwanza, na sikujuwa kama kila nilichokuwa na kifanya kilikuwa ni sahihi. Alipofikia umri wa miezi 18 nilibaini kuna kitu hakipo sawa, lakini sikujua ni kitu gani. Alikuwa anazungumza maneno machache – jambo ambalo niliona ni sawa. Lakini hakuwa akicheza vizuri, alikuwa anavunja vitu na hakuna chochote alichopenda kuchezea kwa muda mrefu. Nikadhani huenda kuna kitu ninakosea'. Alipofikia umri wa miaka 3 mama yake alibaini kuwa mahusiano yake na wanafunzi wengine yalikuwa si mazuri. Alibaini kuwa mwanawe huchanganya maneno na hushindwa kufahamu baadhi ya vitu, lakini alikuwa hajui afanyeje.

Yasmin alipoanza skuli ya msingi, mwalimu wake hakupendezwa na tabia yake na alimuumiza mama yake kwa kumshuku hampi malezi mazuri. Kwa muda wa miezi 18 sasa Yasmin yupo nje ya skuli baada ya kutolewa na mama yake.

### Jadili

- Ni yepi mahitaji ya Yasmin?
- Mbinua zipi zinaweza kusaidia kukidhi mahitaji hayo?
- Uongozi wa skuli/Kamati ya elimu mjumuisho ya skuli ifanye nini?
- Kwa njia gani Jumuiya ya Watu wenye Ulemavu inaweza kusaidia kwa ufanisi uhamaji wa mtoto?

## Kielelezo nam. 6.2: Misingi ya kuzingatia ili kufanikisha uhamaji usio na usumbufu

- Wanafunzi wote wanastahiki na wanapaswa kuhakikishiwa uhamaji usio na usumbufu.
- Uhusiano mzuri ni muhimu: Uhamaji wenye ufanisi huhusisha kuaminiana baina ya pande mbili na kuheshimiana baina ya mtoto, mzazi na watendaji wote wanaohusika.
- Kila mwanafunzi ni wa pekee: usaidizi unaotolewa unapaswa kuwa uliorekebishwa kwa kuzingatia mahitaji ya mwanafunzi.
- Usaidizi ulioratibiwa na mawasiliano mazuri baina ya walimu na taasisi nyengine ni muhimu.
- Mazingira ya skuli yanaruhusu mawasiliano yalio wazi, ya kuaminika na ya dhati na yanashajiisha ushirikiano.
- Muda wa kutosha na rasilimali zinatengwa ili kuhakikisha udahili, tathmini ya awali (usaili) na msaada wa utambulisho wa awali katika mazingira ya skuli ni wenye ufanisi.
- Wanafunzi wanasikilizwa, bila kujali ni wadogo kiasi gani, ili mahitaji yao yafahamike na maoni yao kuzingatiwa.
- Familia zinahusishwa katika kupanga: wazazi/walezi ni chanzo muhimu cha taarifa na msaada kwa skuli.

## Kielelezo nam. 6.3a: Kadi za changamoto

Nakili na kata seti ya kadi hizi kwa kila kikundi kidogo kilichoundwa. Zingatia kuwa katika kadi isiyo na maandishi, walimu wanaweza kuandika changamoto za ziada, iwapo watazibaini wakati wa mjadala.

| | |
|---|---|
| Sioni njia hapa au hamna njia inayopitika kwenda katika skuli yangu mpya. | Kama mtoto wa kike, hivi sasa nimekuwa, inanipasa kufanya kazi zaidi za nyumbani. Hii husababisha nichelewe skuli na hujikuta matatani. |
| Ratiba mpya inanichanganya. Natakiwa niende wapi na saa ngapi? Nagombwa kwa kuchelewa. | Skuli yangu mpya ipo mbali na ninapoishi na inanibidi niende skuli peke yangu, lakini njia sio salama. |
| Wazazi wangu hawajui kuwa napaswa kufanya kazi za nyumbani ninaporudi nyumbani. Wanataka muda wote nimlee ndugu yangu na kufanya kazi nyengine nyumbani. | Walimu katika skuli yangu niliyotoka walipanga jinsi ya kunisaidia katika baadhi ya masomo. Skuli yangu mpya haitambui hili. Mipango yote ya kusaidiwa inabidi ifikiriwe upya. Natamani mwalimu wangu wa zamani angehusishwa. |
| Wazazi wangu hawajali kuhusu masuala yangu ya skuli tangu niingie madarasa ya juu, lakini bado ningependa wazungumze na walimu wangu ninapokuwa na matatizo. | Walimu wanafanya mambo tofauti na nilivyozoea katika skuli hii. Wana mbinu tofauti za kufundishia. Nashindwa kujua matarajio yao. |
| Nilichekwa siku ya kwanza nilipokwenda skuli kwa sababu sikuwa na koti. | Sijazoea kuwa mbali na wazazi wangu siku nzima. |

| | |
|---|---|
| Masomo yanachosha. Nasoma masomo yaleyale niliyosoma katika skuli yangu ya awali. | Kila mtu anahisi nimeshakuwa mkubwa na ninaweza kuzoea katika skuli yangu mpya. Bado naogopa na najisikia kuchanganyikiwa. |
| Nataka kujiunga na chuo cha mafunzo ya amali. Sijui vyuo gani ni jumuishi kwa wanafunzi wenye ulemavu. Pia hakuna mtu yeyote anayejua katika skuli yangu. | Sikuwahi kuona jinsi ilivyo ndani skuli yangu mpya siku niliokwenda kuanza muhula wa kwanza. Nilikuwa naogopa. |
| Nimeingia matatani kwa kuonekana jeuri kwa mwalimu wangu mpya kwa sababu sifahamu anachotaka nifanye. | Nina wasiwasi sitopata marafiki wapya au kuweza kushiriki ipasayo katika mambo ya skuli. |
| Sijisikii kuwa sehemu ya skuli hii. | Nachokozwa na huwa na hofu hasa wakati wa mapumziko na chakula cha mchana. |
| | *Kadi tupu kwa ajili ya washiriki kuandika changamoto za ziada* |
| | |
| | |

# Kielelezo nam. 6.3b: Kadi za mikakati

Nakili na ukate seti ya kadi hizi kwa kila kikundi. Kumbuka kuwa zinapaswa kuwa kadi zenye rangi tofauti na za **Kielelezo nam. 3.2.** Katika kadi zilizokuwa hazijaandikwa, washiriki wanaweza kuandika mbinu za ziada, iwapo watabaini yoyote wakati wa mjadala.

| | |
|---|---|
| Watembeze wanafunzi wapya kuona mazingira ya skuli, wape ramani na andaa usaidizi rika (kwa mfano, 'rafiki wa darasani' ) kumsaidia ajuwe njia. | Wahusishe wazazi/walezi mapema utakapokuwa unaandaa mpango wa maendeleo ya mwanafunzi mmoja mmoja na mpango wa uhamaji. Wape wazazi/walezi vipeperushi vinavoelezea watarajie nini na mambo ambayo wao na skuli inaweza kuyafanya ili kurahisisha mchakato wa uhamaji. |
| Hakikisha kuna usaidizi rika kwa wanafunzi wote wapya kwa wiki kadhaa, na kwamba wanafunzi wote wajuwe kuwa wanatakiwa kusaidiana wao kwa wao na kushukuriana kwa kusaidiana. | Wawezeshe walimu kuwatembelea baadhi ya wanafunzi ili kujuwa mahitaji yao, familia na mfumo wa usaidizi wa jamii. |
| Kwa uchangamfu wakaribishe wazazi/walezi wote na andaa mkutano wa udahili ambapo taarifa zinaweza kutolewa kabla watoto wao hawajawasili skuli.<br><br>Wakaribishe tena wazazi/walezi wa wanafunzi wapya baada ya wiki chache ili kuwapatia ripoti ya maendeleo ya awali na kuelezea matarajio ya skuli. | Kwa haraka wapongeze wanafunzi wapya pale wanapoonesha juhudi au kwa jambo lolote wanalofanya vizuri na kwa utulivu wao.<br><br>Endeleza msaada wa kurahisiha mchakato wa uhamaji kwa kipindi cha mwaka mzima kwa wanafunzi watakaouhitaji msaada huo |

| | |
|---|---|
| Wakaribishe wazazi/walezi darasani (hasa katika madarasa ya awali na ya mapokezi) ili kuwafariji (kuwatuliza ) watoto wao. | Washirikishe wazazi/walezi utakapokuwa unaandaa mpango wa uhamaji na shughuli. |
| Hakikisha kuna wafanyakazi wanaoratibu mchakato wa kuhama kutoka darasa/skuli. | Dumisha mawasiliano kuwasaidia wanafunzi kabla, wakati na baada ya kuhama. |
| Rekebisha mtaala na mbinu za kufundishia ili kufahamu uzoefu wa wanafunzi wapya katika skuli yao ya mwisho kabla ya kujiunga na skuli yako. | Andaa ziara za walimu baina ya skuli. Kwa mfano, mwalimu wa skuli mpya ambaye anahusika na mwaka wa mwisho wa kumaliza wanafunzi kabla ya kwenda skuli nyengine, pamoja na mratibu wa elimu mjumuisho, wanaweza kutembelea madarasa ya wanafunzi wanaotarajiwa kumaliza ili kuwajua na kujibu maswali yao. |
| Hakikisha mipango binafsi ya elimu inahifadhiwa na kukabidhiwa kwa mwalimu/skuli mpya anayokwenda mwanafunzi. | Andaa mpango thabiti wa tathmini ya awali na weka malengo machache ya muda mfupi ya kijamii na kitaaluma kwa kila mwanafunzi mpya, ukikagua maendeleo kila baada ya wiki chache. |

| | |
|---|---|
| Hakikisha skuli za sekondari zina taarifa kuhusu skuli/vyuo mbadala vinavyofikika/ vilivyo jumuishi. | Hakikisha skuli za sekondari, sekondari za juu na taasisi za mafunzo ya amali vinatoa muongozo wa kozi za kusomea huku zikitoa ushauri sahihi na wa kuhamasisha kwa wanafunzi wenye mahitaji maalumu na ulemavu. |
| Msaidie mwanafunzi pale anapokuwa hajafahamu; tarajia baadhi ya wanafunzi wapya kuwa wazungumzaji sana au wenye kelele wanapokuwa na hofu au wamefurahi katika mazingira yao mapya. | Hakikisha wanafunzi wote wapya wanashiriki katika shughuli za ubunifu na burudani yaliomo kwenye mtaala na shughuli za nje ya skuli ili kwa haraka waweze kuzoeana na jamii, kufurahi na kutambua lengo la uwepo wao na kupiga hatua. |
| Wasaidie wanafunzi kutembelea darasa/skuli yao mpya na kujua mazingira, watu na taratibu kabla hawajajiunga rasmi na skuli hiyo. | Hakikisha walimu wanatambua kikamilifu historia ya kujifunza ya kila mwanafunzi, ikisaidiwa na tathmini ya awali waliofanyiwa wanafunzi. |
| Hakikisha mahitaji yote ya mwalimu kitaaluma yanapatikana ili kuhakikisha wanafunzi wake hawajisikii wametengwa au kuwa tofauti na madarasa mengine. | Andaa hafla za kujenga urafiki katika wiki chache za awali za masomo. |

| | |
|---|---|
| Andaa 'siku za utambulisho' wakati wa muhula kabla ya kuhama. Katika siku hizi wanafunzi wapya watakutana na walimu watakaowasomesha mwaka ujao na kujionea baadhi ya masomo yakiendelea, wapate fursa ya kuonana na baadhi ya wanafunzi wenzao kutoka skuli nyengine ambao watakuwa nao pamoja na kuwauliza wanafunzi ambao walikuja kutoka katika skuli zao mwaka uliopita. | Wasaidie wanafunzi wapya kusimamia mchakato wao wa kujifunza na kwa pamoja watafakari kuhusu uzoefu wao wa kuhama. Baadhi ya skuli zilifanya mijadala mizuri wa mafanikio iliyolenga kujua kuhusu vipi wanafunzi hujisikia na inakuwaje anapohamia skuli nyengine. |
| Andaa sera ya kupinga/kupiga vita ukatili na hakikisha watu wanaoshughulikia muda wa mapumziko na wakati wa chakula cha mchana wanapewa taarifa kama kuna wanafunzi wowote wapya. | Wafundishe wafanyakazi wote jinsi ya kusaidia kutatua mahitaji ya mwanafunzi ya kisaikolojia, kimwili na kitaaluma wanapoondoka au kujiunga na skuli na wapatie miongozo. |
| Hakikisha bidhaa za akiba nguo/sare zinakuwepo kwa ajili ya wanafunzi wanaotoka katika familia masikini. | Andaa michezo/shughuli zilizoratibiwa wakati wa mapumziko/wakati wa chakula cha mchana. |

| | |
|---|---|
| Hakikisha kuwa wanafunzi wapya wanapangiwa majukumu mapema na kwamba washirikiane na wanafunzi wazoefu, yakijumuisha shughuli za michezo, klabu (vikundi) na uandaaji wa michezo ya shule. | Wasikilize wanafunzi wapya na wakufunzi wao. Andaa vikao vya mapitio/tathmini baada ya wiki chache za awali. Wao ndio wenye uzoefu kamili kuhusu hali wanayoipitia wakati wa kuhama kutoka skuli moja kwenda nyengine na kwa hivyo wapo katika nafasi nzuri ya kutuambia aina gani ya msaada wao na wenzao wanauhitaji. |
| Hakikisha kila mmoja anajua aende wapi (hasa wakati wa mapumziko) kama hawajisikii salama. | *Kadi siyo na maandishi kwa ajili ya washiriki kuandika mikakati ya ziada* |
| | |
| | |